SportPesa
JACKPOT BABA LAO!
TZS. 253,545,950
CHEZA SASA KWA 1000/= TU!
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Utata** kifo cha kijana aliyepigwa risasi mgodini

UKURASA 4



**JUSTIN BIEBER APOOZA USO**

UKURASA 20


# Nipashe Jumapili

MWANGA WA JAMII

Jumapili Juni 12, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580974

www.ippmedia.com

witter.com/nipashetz | www.facebook.com/nipashetz | www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




# Askari auawa kwa mshale Loliondo

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**IGP AAGIZA MSAKO MMILIKI GARI AJALI ILIYOUA WATU 20**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Saimon Sirro, ameagiza mmiliki wa gari aina ya...

UKURASA WA 7

**HALMASHAURI ZAPEWA MWEZI KUPIMA ARDHI**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula ametoa...

UKURASA WA 7

**AJALI YAUA WATANO WAKIENDA MSIBANI**

WATU watano wamefariki dunia papo hapo na wengine tisa kujeruhiwa baada ya basi...

## Migogoro ya ndoa chanzo ugonjwa akili

UKURASA 8



Rais Samia Suluhu Hassan akishuhudia utiaji saini wa makubaliano ya awali ya mkataba wa nchi hodhi (HGA) wa mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma jana. Wanaotia saini ni Waziri wa Nishati, Januari Mkamba (wa pili kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dk. James Mtaragio na Makamu wa Rais na Mwenyekiti wa Tanzania Equinor AS, Unni Merethe (kulia) na Makamu Rais wa kampuni ya Shell Exploration, Jared Kuehl. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Samia atangaza neema ajira maelfu gesi asilia

UKURASA 2

MICHEZO **VITA KALI UCHAGUZI MKUU YANGA** UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, akikata utepe kuzindua kituo kidogo cha Polisi Ghymkhana, Kata ya Kivukoni, jijini humo juzi, baada ya kukarabatiwa na kampuni ya Dezo Construction. Wengine ni Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Premji Pindoria (wa pili kushoto), Diwani wa kata hiyo, Sharik Choughule (wa tatu kushoto) na (wa pili kulia) ni Kamanda wa Polisi Mkoa wa kipolisi Ilala, Debora Magiligimba. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Samia atangaza neema ajira maelfu gesi asilia

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa maagizo sita kwa watendaji serikalini, sekta binafsi na wananchi katika kuchangamkia fursa ya mradi wa kuchakata gesi ya Mtwara na Lindi ambao mazungumzo ya awali yatakamilika Desemba mwaka huu na kuanza utekelezaji.

Vilevile, mradi huo unatarajiwa kutoa ajira 10,000 kwa kipindi cha ujenzi na baadaye za kudumu 500 na ndiyo sababu ya uamuzi wa serikali wa kuanzishwa kanda maalum ya kiuchumi kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vyenye muunganiko na mradi.

Mkuu wa Nchi alibainisha hayo jana Ikulu Chamwino baada ya kushuhudia utiaji saini wa makubaliano ya awali ya mkataba wa mradi wa nchi hodhi wa kuchakata na kusindika gesi ya LNG baina ya Wizara ya Nishati, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na kampuni za Shell na Equinor zilizogundua nishati hiyo kwenye kitalu namba moja, mbili, nne na kina cha Bahari ya Hindi.

Alisema mradi huo wa kimkakati ni mahususi kwa kuwa unaleta mtaji na mapato nchini na kwamba utakapokamilika utabadilisha taswira ya uchumi wa nchi, huku akitoa maelekezo sita.

Rais katika agizo lake kwa kwanza, aliwataka watendaji wanaohusika kwenye majadiliano, kusimamia maslahi ya nchi kwa kuhakikisha kunakuwa na wepesi kwa kila upande.

La pili, mikoa ya Lindi na Mtwara kujiandaa kuzitumia fursa zitakazoletwa na mradi katika kukuza kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Tatu, Rais aliagiza mchakato wa majadilino na makubaliano ujenge uwezo wa Watanzania ili vizazi vijavyo vivune kwa tija na kujitegemea zaidi.

Nne, lazima kujenga uwezo wa Watanzania kushiriki kikamilifu na kutumia manufaa ya mradi na kwamba mafuta na gesi ni biashara na uwekezaji mkubwa unaohitaji kuimarisha taasisi za umma ili kusiwe na kikwazo kwa kuwa walindaji wa mradi ni Watanzania na siyo wawekezaji.

La tano, TPDC ndiyo wabia, hivyo wanapaswa kuwa shirika la kimkakati kwa nchi ili miaka ijayo shughuli hizo wazifanye wenyewe, Rais Samia akifafanua kuwa uzoefu wa sasa unaonyesha hakukuwa na wataalamu wa kutosha hadi wakatafutwa kwingine.

"Huko mbele tuwe nao na ndiyo maana nimeweka Mwenyekiti wa bodi nzito, Balozi Ombeni Sefue, atakayeweza kusimamia vyema TPDC, pia waziri naye ameweka bodi nzuri.

"TPDC kazi iko kwenu, nyie ni wachezaji, tunategemea magoli mengi kutoka kwenu, iwapo hamasa. Wizara ya Nishati wakae na Wizara ya Fedha waone namna gani ushiriki wa TPDC uwe wenye manufaa, tumewapa kazi, lazima wapewe nyenzo za kuifanya kazi vizuri," aliagiza.

Katika agizo lake la sita, Rais Samia alisema Watanzania wajipange kunufaika na fursa kwa kuwa mbali na mtambo wa kuchakata gesi, kutakuwa na kanda maalum ya uchumi, hivyo sekta binafsi lazima ijipange kutoa huduma kwenye mradi, kuhudumia mradi wenyewe katika kukuza uchumi badala ya kusubiri watu wa nje waje kutoa huduma kwenye mradi na kupeleka mapato kwingine.

"Sekta binafsi ihusike kwa sababu uzoefu unaonyesha maeneo ambayo serikali inaendesha yenyewe, hakuna utekelezaji mzuri. Kutia saini mkataba haina maana uwekezaji utaanza kesho kwa kuwa bado kuna vipengele vinahitaji mjadala, ni matumani ikifika Desemba mwaka huu tutasaini makubaliano ya pili mradi uanze na kwenda kwenye hatua nyingine," alisema.

Kwa mujibu wa Rais Samia, mradi huo utagharimu Sh. trilioni 70 na asilimia 10, yaani Sh. trilioni saba zitatumika ndani kwa ununuzi na kutoa huduma ndani ya nchi na hivyo kuwa fursa pana kwa Watanzania kiuchumi.

Alisema kuna fursa nyingine ya mradi kwa gesi kutumika nyumba na kwenye huduma za kijamii na maboresho makubwa yatafanyika kwa Uwanja wa Ndege Mtwara, barabara na huduma za kijamii kwa kuwa na shule, vituo vya afya vizuri, maji na umeme.

Awali Waziri wa Nishati, January Makamba, alisema ugunduzi huo wa gesi ulifanyika kwa kushirikiana na washirika na TPDC, serikali ikifanya uamuzi wa kuanza mradi wa kusindika na kuchakata gesi asilia kutoka kwenye hali ya hewa kwenda kwenye kimiminika kwa ajili ya kuuza nje na kutumia nyumbani.

"Utekekezaji mwa mradi huu Lindi utafanyika sambamba na uendelezaji wa miundombinu ili kuwezesha kuvuna rasilimali hiyo kwa ajili ya uendelezaji, tutajenga mtambo nchi kavu tofauti na nchi nyingine wanajenga kilipo kisima kwa kuweka meli ichakate na kusafirisha duniani.

"Tunajenga miundombinu kutoka nchi kavu itakapokuwa mtambo kwenda kilomita 100 hadi 160 halafu tunaenda kilomita tatu kufikia sakafu ya bahari na kuchimba kilomita mbili zaidi iliko gesi.

"Ni mradi mkubwa utakaobadilisha sura na taswira ya nchi, tumepata eneo Likongo, Mto Mkavu na Masasi ya leo mkoani Lindi tumeshalipa fidia kwa maridhiano kwa kaya 642 na tayari serikali ina hati.

"Uwekaji saini wa masuala muhimu yaliyokubalika katika hatua za awali na mengine yatawezesha usanifu wa kihandisi kufikia uamuzi wa mwisho ya uwekezaji mwaka 2025.

"Tanzania tuna visima 34 vya mafuta na gesi, vitalu 22 hakuna kinachoendelea, vitalu 12 ndiyo kuna shughuli, tunaamini mwaka ujao wa fedha na unaofuata kutokana na shughuli hii na hamasa, tutapata watu wengi zaidi kuja kuwekeza," alisema.

Waziri huyo alisema dunia inahama kutoka kwenye gesi chafu kwenda safi na ya Tanzania ni asilia ambayo ni chafu kidogo, inayofaa kutumia kipindi cha mpito duniani, akiyataja masoko ya China, India, Korea na Japan ambayo kijiografia ni rahisi kuyafikia.

Wawakilishi wa kampuni za Equinor na Shell, walisema zaidi ya Sh. trilioni tisa zimewekezwa kwenye utafiti wa kiwango cha gesi asilia na ili kuifikisha nishati kwenye masoko makubwa duniani, ni lazima kufanya uwekezaji mkubwa kwa kujenga miundombinu nje na ndani ya bahari.

# Askari auawa kwa mshale Loliondo

**Na Waandishi Wetu,** ARUSHA

SERIKALI mkoani Arusha imetoa taarifa kuwa askari mmoja amefariki dunia kwa kuchomwa na mshale kutokana na vurugu ambazo zilijitokeza wakati wa uwekaji wa mipaka katika eneo la Pori Tengefu la Loliondo lililoko wilayani Ngorongoro mkoani hapa.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alitoa taarifa hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelezea kinachondelea Loliondo katika utekelezaji wa kuweka mipaka kwenye eneo hilo.

"Bahati mbaya tu alasiri ya jana (juzi) askari wetu mmoja aliuawa kwa kupigwa mshale na kundi la watu ambalo lilitokea na kutaka kuathiri zoezi na hata kuumiza waliokuwa wakiendelea na zoezi, ni bahati mbaya sana lakini askari mzalendo tunatambua mchango wake," alisema.

Hata hivyo, Mongella hakueleza kwa kina taarifa kuhusu askari huyo na hata Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, alipotafutwa mara kadhaa ili kutoa ufafanuzi zaidi askari aliyeuawa, hakupatikana kwa simu.

Mongella alisema kimsingi uwekaji mipaka katika eneo hilo unaendelea vizuri na kwamba vyombo vya ulinzi na usalama vipo timamu kwa ajili ya kulinda zoezi lenyewe lakini hata wananchi wa maeneo hayo maana ndio wajibu wa vyombo vya ulinzi na usalama.

Alisema pamoja na kuwapo kwa picha nyingi zinazorushwa mitandaoni zikionyesha watu waliojeruhiwa, mpaka sasa kwenye hospitali na vituo vya afya hakuna majeruhi.

"Tumeona kwenye mitandao kuna picha zinatolewa, bahati mbaya sana baadhi ya picha ni za miaka mingi iliyopita, kuna picha zimetambulika za miaka mitatu, minne iliyopita," alisema.

Mkuu wa Mkoa, alitoa wito kama kuna mtu yeyote ana jeraha kutokana na chochote anadhani kimesababishwa na vyombo vya ulinzi na usalama au mamlaka, ajitokeze ili apate huduma kwa sababu huo ndiyo mwelekeo wa serikali.

"Serikali yetu ni serikali ya utawala wa sheria na misingi ya utawala bora na tungependa suala la upotoshaji lisiendelee sababu tunafanya jambo ambalo ni la kimaendeleo kwa mstakabali wa wananchi, jamii na maslahi mapana ya nchi yetu," alisema.

Aliongeza kuwa kinachotegemewa na serikali baada ya kuweka mipaka maeneo hayo ili kuimarisha uhifadhi ni kuona ya uhifadhi wa eneo hilo yatakuwa shirikishi.

"Jana (juzi) tunamshukru Waziri Mkuu asubuhi alitoa kauli ya serikali ambayo iliwahakikishia wananchi wa Loliondo na vijiji vinavyozunguka eneo hilo kuwa serikali iko nao na wao ni mashahidi wa juhudi kubwa zinazofanywa na serikali kwa ajili ya maendeleo yao," alisema.

Katika Wilaya ya Ngorongoro kuna kilometa za mraba 4,000 ambazo mwaka 1951 ilipitishwa kama sheria kwamba eneo hilo ni eneo la Pori Tengefu la Loliondo.

Hata hivyo, serikali kwa kuguswa na maendeleo ya watu wake na baada ya wananchi kuingia eneo lile, iliamua eneo hilo litengwe kilometa za mraba 2,500 wananchi wabaki waendelee na shughuli zao za maendeleo na serikali iweke nguvu kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya uhifadhi eneo la kilometa za mraba 1,500.

■**Imeandikwa na Novatus Makunga na Thobias Mwanakatwe, ARUSHA**




Mafundi wakiendelea na ujenzi wa Barabara inayounganisha eneo la Matosa na Goba njia nne kwa kiwango cha lami, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# IGP aagiza msako mmiliki gari ajali iliyoua watu 20

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Saimon Sirro, ameagiza mmiliki wa gari aina ya coaster lililosababisha vifo vya watu 20 wilayani Mufindi mkoani Iringa, kusakwa ili kuchukuliwa hatua za kisheria kwa kuruhusu basi lake kufanya kazi ya kubeba abiria bila kuwa na kitabu cha tiketi.

"Hataruhusiwa kuchukua gari lake polisi hadi atakapopatikana ili atueleze aliruhusu vipi gari lake kufanya kazi ya kubeba abiria bila kuwa na kitabu cha tiketi," aliagiza.

IGP Sirro pia alipiga marufuku magari yasiyo ya abiria kubeba abiria na kuwa msako mkali utafanyika ili kuchukua hatua zaidi.

Akizungumza jana mjini Iringa baada ya kuwatembelea majeruhi wa ajali hiyo waliolazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa, IGP Sirro alisema kuwa Jeshi la Polisi limejipanga kuchukua hatua kali dhidi ya madereva wasiofuata sheria na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi aliwataka Watanzania kutokubali kupanda basi lolote ambalo halitoi tiketi kwa abiria wake.

Alisema sheria inawataka wenye vyombo vya kusafirisha abiria kutoa tiketi kwa wasafiri na kutofanya hivyo ni kosa kisheria.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Iringa, Jasmine Kachemela, alisema hadi jana mchana, majeruhi wanne walikuwa wamepokewa kutoka kwenye ajali hiyo iliyosababisha vifo vya watu 20 na majeruhi saba.

Alibainisha kuwa kati ya majeruhi hao, mmoja yupo mahututi na kwamba maiti zilizokuwapo zilikuwa tisa, zikiwamo saba ambazo zilikuwa hazijatambuliwa.

## Mbaroni tuhuma wizi wa ng'ombe

**Na Neema Hussein,** KATAVI

Jeshi la Polisi mkoani Katavi linawashikilia watu watano wakituhumiwa kuiba ng'ombe 33 katika matukio tofauti.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi mkoani Katavi, Ali Makame, alisema tukio hilo limeripotiwa kutokea Kijiji cha Lwega wiyani Tanganyika.

Makame alisema kuwa Juni 4 mwaka huu, Samweli Simon, mkazi wa kijiji hicho, aliripoti kuibiwa ng'ombe 28 wakiwamo majike 16 na madume 12 na kwamba wezi hao walivunja zizi na kuwatoa kisha kutokomea nao kusikojulikana.

Katika tukio hilo, aliwataja watuhumiwa watatu waliokamatwa na ng'ombe 10 wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni sita kuwa ni Masanja Peter, James Mayuya na Jihumbi Tungu, wote wakazi wa Kijiji cha Gagala.

Alisema jeshi hilo linaendelea kuwasaka watuhumiwa wengine wanaodaiwa kuwa na ng'ombe 18 waliobaki na kwamba baada ya upelelezi kukamilika watuhumiwa watafikishwa mahakamani.

Watuhumiwa wengine wawili Daud Nsola (29), mkazi wa Kijiji cha Ilalangu wilayani Mlele na Keya Juma, mkazi wa Chamalendi, wanadaiwa kuiba ng'ombe watano wenye thamani ya Sh. milioni nne wakiwa wanatoka malishoni, mali ya Robart Lume, mkazi wa kijiji hicho.

Kamanda Makame alisema polisi baada ya kupata taarifa, kwa kushirikiana na raia wema na sungusungu, walifanikiwa kuwakamata ng'ombe hao wakiwa wamefichwa Kijiji cha Mirumba na watuhumiwa.

# HESLB yazindua mfumo wa kidigitali kurejesha mikopo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imezindua rasmi mfumo wa kidigitali unaomwezesha mwajiri kuwasilisha makato na orodha ya wanufaika-wafanyakazi wake kwa njia ya mtandao kutoka popote alipo.

Akizindua mfumo huo jijini Dodoma juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, alisema mfumo huo ulianza kwa majaribio mwaka 2019/20 na sasa umekamilika na hivyo kuwawezesha waajiri na wanufaika kurejesha mkopo kwa urahisi.

"Zamani ilikuwa mwajiri inabidi atoke ofisini kwake aje HESLB kufanya malipo lakini kwa sasa anaweza kuwasilisha orodha ya wanufaika-wafanyakazi wake na makato kutoka popote alipo kwa kutumia mfumo wetu huu ambao anajiunga kupitia tovuti yetu (www.heslb.go.tz)," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji huyo alisema mfumo huo pia unamwezesha mnufaika mmoja mmoja kupata taarifa za deni lake na utaratibu wa kurejesha kupitia tovuti ya HESLB.

"Kuanzia mwaka jana, imekuwa ni rahisi sana, unaingia kwenye tovuti yetu, unabofya 'rejesha mkopo' au 'repay loan' na kufuata maelekezo ya kujisajili na utaendelea kupata taarifa ya deni lako palepale au hata kudai refund (makato yaliyozidi)," alisema.

Akizungumzia uzoefu wake katika kutumia mfumo huo, mwakilishi wa Shule ya Msingi Young Jai iliyoko Dodoma, Young Mi Cha, aliishauri HESLB iboreshe mfumo kuwawezesha waajiri kuwatambua waajiriwa wapya kama walinufaika na mikopo ya elimu ya juu.

"Kuna wakati waajiriwa wapya wanadanganya, hivyo pamoja na uzuri wa mfumo huu, ninashauri uboreshwe ili mwajiri aweze kutambua mwajiriwa mpya kama ni mnufaika wa HESLB au hapana bila kumuuliza au kuleta jina kwenu kwa uhakiki kwanza," alishauri Young.

HESLB ilianzishwa mwaka 2005 ikiwa na majukumu makuu mawili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji wanaojiunga na taasisi za elimu ya juu na kukusanya mikopo iliyoiva kutoka kwa wanufaika

**KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI**

**DEOGRATIAS MUMENYA MWIJAGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji aina ya **TVS KING** yenye namba za usajili **MC 288 BUQ,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa

**MBE/MBE/RB/226101/2022**

# DED apewa miezi miwili kumaliza ujenzi zahanati

**Na Friday Simbaya,** KILOLO

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, amempa miezi miwili Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, Laini Kamendu na timu yake kuhakikisha ujenzi wa kituo cha afya na zahanati mbili unakamilika, kuwekewa samani na kuanza kutumika.

Sendiga aliagiza hayo jana wakati wa kikao cha Baraza Maalum la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo chenye lengo la kujibu hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2020/21 kwa halmashauri hiyo.

Alisema kuna Kituo cha Afya cha Ng'uruwe, Zahanati za Mbawi na Lugalo zimekamilika lakini mpaka sasa hazijaanza kufanya kazi.

Alisema kupitia taarifa iliyotolewa na CAG, inaonyesha bado kituo cha afya na zahanti mbili hazijaanza kutumika licha ya majengo kukamilika.

Sendiga alifafanua vituo hivyo vya kutolea huduma za afya bado havijawekewa samani za ndani ili kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

"Wananchi wanaposikia kuna ujenzi wanafurahi kwa kuchangia nguvukazi zao ndio maana wanaleta maji, mawe na mchanga wakitegemea ujenzi ukikamilika wataanza kupata huduma," alisema Sendiga.

Mkuu wa Mkoa pia aliitaka Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo kuzifanyia kazi haraka iwezekanavyo hoja 18 zilitolewa na CAG pamoja na kuwachukulia hatua wale wote waliosababisha upungufu huo.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Anna Msolla, aliwataka wataalamu wake kuzingatia maelekezo yote yaliyotolewa na serikali kwa kufuata kanuni na miongozo.

Alisema kuwa CAG aliibua hoja mbalimbali katika halmashauri hiyo zinazojumuisha taarifa za kitabu kikuu. Msolla alisema katika ukaguzi huo wa serikali, CAG alitoa hati inayoridhisha kwa halmashauri ya wilaya hiyo katika mwaka wa fedha wa 2020/21

Aliendelea kusema katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2015 hadi 2020, halmashauri ya wilaya hiyo ilikuwa na hoja 23 na 2019/20 hoja 13 zilisalia katika ripoti iliyotolewa katika mwaka wa fedha 2020/21.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Iringa, Happiness Seneda, aliomba timu ya menejimenti kwamba hoja hizo zifungwe na zitakazosalia ziendelee kufanyiwa kazi kabla ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2021/22.

Alifafanua kuwa, ukaguzi wa hesabu wa mwaka 2020/21 halmashauri ya wilaya hiyo ilikuwa na hoja mpya 30, ikiwa ni ongezeko la hoja 10. Seneda aliipa siku 10 timu ya menejiment ya halmsahuri hiyo kuhakikisha hoja hizo zimefanyiwa kazi na kupungua kabla ya kikao cha tathamini cha mkoa cha halmashauri zote za mkoa huo Juni 20 mwaka huu.

Alifafanua kuwa kifungu 45 cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982, kinataka kila baada ya kuisha mwaka wa fedha, taasisi zote za serikali lazime zifunge hesabu zake na kuziwasilisha kwa CAG kwa ajili ya ukaguzi.

Alieleza zaidi kuwa katika mwaka wa fedha 2020/21 halmashauri hiyo ilifunga hesabu zake na kuwasilisha kwa CAG kwa ajili ya ukaguzi na katika mwaka huo wa ukaguzi, halmshauri ilipata hati inayoridhisha.




Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja Vodacom Tanzania Plc, Harriet Lwakatare (katikati), akionyesha tuzo ya kampuni Bora kwa Huduma kwa Wateja, iliyotolewa na Taasisi ya Serengeti Bytes, kupitia tuzo zake za Tanzania Digital Awards, ambapo kampuni hiyo, ilishinda kutokana na huduma bora za kidigitali kwa wateja, ambazo ni matokeo ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Vodacom. Kushoto ni Mkurugenzi wa kitengo cha dijitali na huduma za ziada Vodacom, Nguvu Kamando na Ofisa Uendeshaji wa Serengeti Bytes, Michael Mallya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Utata watawala kifo cha kijana kwa risasi mgodini

**Na Waandishi Wetu**

UTATA umetawala mkasa wa kifo cha kupigwa risasi kijana wa umri wa miaka 23, Cosmas Hamisi, ukiacha maswali kutoka hoja zinazokinzana kuhusu namna ya kifo chake, mazingira halisi na jinsi alivyohudumiwa.

Wakati wazazi wanadumu katika hoja mtoto wao aliuawa nje ya mpaka wa mgodi wa almasi wa El-Hilali wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, ufafanuzi wa Jeshi la Polisi unasimamia mauaji yaliyotokea ndani ya mgodi huo mnamo Machi 10 mwaka huu.

Vilevile, mazingira ya kupigwa risasi kwake yameripotiwa na polisi kwamba kijana huyo alikuwa akipambana na askari polisi kutaka kumpoka silaha yake, ilhali ufafanuzi wa kifamilia ni kwamba alipigwa risasi umbali mrefu kutoka alikokuwa askari mwenye silaha.

Eneo lingine la swali linalojitokeza katika kifo cha Cosmas, ni maelezo yanayopishana kuhusu fedha Sh. 100,000 zilizotolewa kukimu maziko yake, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, George Kyando, akiiambia Nipashe zilitolewa na mgodi, huku Kaimu Meneja wa mgodi huo, Antony Rafael, akikataa wao kutoa fedha hizo.

Hata hivyo, akizungumza na Nipashe, Machi 17 mwaka huu, baba wa marehemu, Hamisi Kushilimwa (50), alisema fedha hizo za kuwasaidia kusafirisha mwili kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, alipewa na Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Shinyanga.

Kuhusu hatua za kisheria, Kamanda Kyando aliiambia Nipashe mwanzoni mwa wiki hii kwamba hakuna hatua zaidi zinazoendelea, kwa kuwa muuaji alikuwa sahihi kisheria.

"Kijana huyo aliuawa na askari ndani ya mgodi huo wakati alipokuwa akitaka kuichukua silaha, ndipo askari akajihami na kufyatulia risasi.

"Hata kama ungekuwa ni wewe ndiyo askari, mhalifu anataka kukupora silaha yako, ungefanyaje? Lazima ujihami, hivyo askari alikuwa sahihi, hapa hakuna kesi," Kamishna Msaidizi Kyando alifafanua.

Hata hivyo, Nipashe ilipotaka ufafanuzi wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni jijini Dodoma Aprili 20 mwaka huu, aliagiza kufanyike uchunguzi kuhusu mauaji hayo.

"Kwenye PGO (Kanuni za Mwongozo wa Utendaji wa Jeshi la Polisi) kumeelekezwa hatua za kufuatwa wakati wa kutekeleza ukamataji wa watuhumiwa. Matumizi ya silaha ni hatua ya mwisho kabisa baada ya mbinu zingine kushindikana.

"Katika hili la mauaji ya mgodini, kuna haja ufanyike uchunguzi ili hatua zichukuliwe dhidi ya askari aliyehusika na mauaji hayo," Waziri Masauni aliagiza.

Ni simulizi ya utata wa kiusalama inayoendelea mgodini El-Hilali, huku kukiwapo madai ya kuwapo matukio ya mauaji mgodini huko na tayari kuna kesi iliyofunguliwa katika ngazi ya mahakama kuu Mei mwaka juzi, inayolalamikia ukiukwaji wa haki za binadamu na orodha ya vifo na madhara ya aina hiyo tangu mwaka 2009.

Vilevile, sasa inatimu wiki ya tatu tangu liliporipotiwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga tukio lingine la mauaji ya kijana Hamisi Mayunga (19) aliyedaiwa kuuawa kwa kupigwa risasi na mlinzi wa mgodi huo kutoka kampuni binafsi ambaye alitoweka baada ya tukio na polisi wanamtafuta.

**HATUA ZINAZOCHUKULIWA**

Kwa mujibu wa Kamanda Kyando, kutokana na kukithiri kwa mauaji ya aina hiyo, Polisi Shinyanga hivi sasa imechukua hatua zinazojumuisha kukumbushana wao polisi na askari wa kampuni binafsi matumizi sahihi ya silaha na mipaka yao kisheria.

Kadhalika, kwa upande wa umma, Kamanda Kyando alisema wanaendelea kutoa elimu ya umma kuhusu usahihi na haki ya mgodi huo katika miliki ya maeneo iliyokabidhiwa kisheria na haki ya kutoingiliwa na umma pasi na kufuata taratibu.

Alidokeza kwamba hadi sasa wanaendelea kukagua weledi wa walinzi na wasiokamilika katika stadi hiyo, wanaondolewa kwa muda ili wakapate mafunzo stahiki.

Nipashe pia ilitua mezani kwa Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, kwa lengo la kupata ufafanuzi wa hatua zinazochukuliwa kukomesha mauaji hayo, kiongozi huyo akisema wanatoa elimu kwa wananchi na hasa vijana ili watii sheria za nchi na kuacha kuingia kwenye migodi hiyo ambayo ipo kisheria.

Alisema vijana na wakazi wengine wa vijiji vinavyozunguka migodi hiyo ya almasi wanapaswa kufuata programu za kiuchumi zinazotolewa na mgodi ili wajipate kipato kuliko kuingia ndani ya migodi hiyo kinyume cha sheria na hata kusababisha mauaji.

"Mikakati iliyopo uongozi wa Wilaya ya Kishapu unatoa elimu kwa wananchi kuacha kuingia kwenye migodi hiyo kinyume cha sheria, wafuate program za kiuchumi ambazo zinatolewa na migodi ikiwamo ya kilimo, biashara na uvuvi," alisema Mkude.

Nipashe ilipohitaji kujua kama kuna msaada wa serikali kwa familia ya kijana Cosmas, hasa mtoto wake mchanga, Mkude alikiri kwamba hadi sasa serikali haijatoa msaada wowote kwa familia hiyo.

# Waona fursa utalii Kagera

**Na Mary Geoffrey**

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi siku ya 'Kagera Dinner Party' itakayofanyika Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama mkoani Dar es Salaam.

Lengo la kuwakutanisha wananchi wa Kagera ni kujadili namna watakavyoweza kutumia jiografia ya mkoa wao kutangaza tamaduni na vivutio vya utalii vinavyopatikana huko.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi, Leah Rugemalira, akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani hapa, alisema lengo kuu ni kutangaza utalii wa mkoa huo.

"Katika siku hii muhimu ya kuwakutanisha Wanakagera wote, Rais Samia anatarajiwa kuwa mgeni rasmi na lengo pia ni kuendelea kutangaza utalii ulipo katika mkoa wetu," alisisitiza.

Leah alisema wananchi wa Kagera hawana utamaduni wa kurudi na kuwekeza nyumbani na wamekuwa hawajui kama kuna vivutio.

"Juni 25 mwaka huu tutakapokutana tutakumbushana kuhusu tamaduni zetu, mila, desturi na vivutio tulivyonavyo," alisema.

Aliongeza kuwa wameamua kuanzisha kampeni hiyo baada ya Rais Samia kuzindua filamu maalum ya Tanzania The Royal Tour ambayo inatangaza utalii uliopo nchini.

Alisema wameamua kumuunga mkono kwa kuona umuhimu wa kutambulisha vivuti vilivyopo Mkoa wa Kagera.

Alisema mbali na kukutana na kula vyakula vya asili, kucheza ngoma zao, wataanza kufanya safari za utalii katika hifadhi za Burigi, Ibanda, Bweranyange na eneo ambako alikuwa akiishi Mtemi Rumanyika. Alisema watakutana kwa siku mbili kuanzia Juni 24 mwaka huu na kwamba hakutakuwa na kiingilio badala yake watauza vyakula vya asili, matunda ya asili, magome ya miti na mikeka.

# Bilioni 15/- kumalizia ujenzi uwanja wa ndege Shinyanga

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, amesema wamepewa na serikali Sh. bilioni 15 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa kiwanja cha ndege kilichoko Ibadakuli, Manispaa ya Shinyanga.

Aliyasema hayo juzi wakati akiwa kwenye mkutano wa hadhara akizungumza na wananchi wa Ngokolo, Manispaa ya Shinyanga.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amefanya mambo makubwa mkoani humo na kuwataka wananchi wapuuze maneno ya upotoshaji kuwa katika utawala wake hajafanya kitu.

Mjema alisema Mkuu wa Nchi amekuwa na mapenzi na wananchi na amemwaga fedha nyingi mkoani humo za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo zikiwamo hizo Sh. bilioni 15 za ujenzi huo wa uwanja wa ndege ambapo Sh. bilioni 3.5 zimeshaanza kufanya kazi na mkandarasi yupo eneo la mradi.

Pia alisema serikali imetoa Sh. bilioni 4.5 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana iliyoko Ndembezi, Manispaa ya Shinyanga ambayo itakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita.

"Ninampongeza Rais Samia kwa kutoa fedha za ruzuku na kupunguza bei ya mafuta hali ambayo imewapunguzia wananchi ukali wa maisha pamoja na kuendelea kushusha bei ya bidhaa mbalimbali," alisema.

Mkuu wa Mkoa pia aliwataka wananchi waendelee kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19 na kujiandaa kushiriki Sensa ya Watu na Makazi iliyopangwa kufanyika Agosti 23 mwaka huu.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Yasinta Mboneko, aliwahakikisha wananchi kuwa serikali itaendelea kutatua matatizo yao ikiwamo migogoro ya ardhi, maji, umeme na miundombinu ya barabara.



Muuguzi wa Kituo cha Afya Ngokolo, Manispaa ya Shinyanga, Odilia Mhela, akiwapatia wananchi chanjo ya UVIKO-19, wakati wa mkutano wa hadhara wa Mkuu wa mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema (hayupo pichani), wa kuhamasisha wananchi kupata chanjo, katika Kata ya Ngokolo, juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# DIT yatengeneza mashine kukabiliana na lishe duni

**Na Sabato Kasika**

TAASISI ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) imetengeneza sampuli ya mashine ya kuongeza virutubisho kwenye unga wa mahindi iitwayo 'Kinyunyizi', ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa vyuo vya teknolojia kubuni mashine za aina hiyo ili kupunguza tatizo la lishe duni nchini.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa ukaguzi wa sampuli hiyo kwenye karakana ya DIT iliyobuniwa na mwanafunzi chuoni hapo, Lucas Sabule, Ofisa Usalama wa Chakula kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Rhoda Kidolezi, alisema lengo la serikali ni kupunguza tatizo la lishe duni.

Alisema baada ya maagizo hayo kutolewa, DIT imekuwa ya kwanza kufanya ubunifu huo na kuvitaka vyuo vingine kuharakisha ubunifu wao.

"Tunataka kupunguza tatizo kuanzia ngazi ya chini ambako kuna mashine nyingi za kusaga unga ambazo ni muhimu kuwa mashine ndogo za kuweka virutubisho kwenye unga," Rhoda alisema. Alisisitiza umuhimu wa vyuo vya teknolojia kujitahidi kubuni mashine za kuongeza virutubisho ili lengo la serikali la kupunguza utapiamlo litimie.

Ofisa Teknolojia wa Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), Selestine Mgoba, alisema ipo haja ya kubuni vitu mbalimbali ili kuendeleza viwanda nchini na kuwataka wataalamu wa ndani kujitahidi kuwa wabunifu. "Kubuniwa kwa sampuli ya mashine ya kuongeza virutubisho kwenye unga kutasaidia kupunguza gharama za kuagiza kutoka nje iwapo itakamilika," alisema .

Mgoba alisema katika ukaguzi wake kwenye sampuli hiyo ya mashine amebaini kuwa imekamilika kwa asilimia 80 na zilizobaki ni kwa ajili ya marekebisho machache. "Mashine kama hii zimekuwa zikiagizwa nje kwa gharama kubwa ya Sh. milioni saba kila moja, lakini hii gharama yake ni Sh. milioni mbili, hivyo tunaweza kuokoa fedha nyingi iwapo zitatengenezwa kwa wingi," alisema.

Meneja Mradi wa Virutubisho wa Taasisi inayojishughuliaha lishe ya Taasisi ya Global Alliance for Improved Nutrition (GAIN), Archad Ngemela, alisema hatua ya ubunifu huo inakwenda sambamba na Mpango Jumuishi wa Lishe awamu ya pili ya mwaka 2021/22 kwenda mwaka 2025/ 26.

Alisema mpango huo unalenga kushirikisha wazalishaji wadogo zaidi wa unga kwa kuendana na Mwongozo wa Lishe shuleni.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Makato haya katika mishahara ya watumishi ni hatari kiutendaji

**JUNI** 1999, Tanzania ilizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ambayo dhima yake kuu ni kupunguza walau nusu ya wananchi wanaoishi katika umaskini na kuwafanya wafike uchumi wa kati kufikia mwaka 2025, yaani miaka mitatu ijayo.

Katika kutekeleza malengo ya dira hiyo, serikali imekuwa na mikakati mingi. Mojawapo ni kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) mwaka 2004, japo ilianza rasmi utekelezaji wa majukumu yake mwaka uliofuata.

Hata hivyo, urejeshaji wa mikopo hiyo umeibua malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali kiasi cha kuilazimu mamlaka ya juu kitaifa, Rais Samia Suluhu Hassan kuingilia kati na kutangaza kufuta baadhi ya tozo.

Shida kuu zilizoibua malalamiko ni pamoja na Mwongozo wa HESLB wa utoaji mikopo na Ruzuku kwa Wanafunzi kutaka mnufaika wa mkopo wa bodi hiyo kulipa tozo ya kulinda thamani ya fedha ambayo ilikuwa inakatwa asilimia sita kwa mwaka tangu tarehe mnufaika aliyoanza kupokea mkopo. Serikali ilifuta makato hayo kuanzia Julai Mosi, mwaka jana.

Mwongozo huo ukaelekeza mnufaika akishindwa kulipa mkopo baada ya kipindi cha neema cha miezi 24 baada ya kuhitimu masomo yake, kuongezwa makato ya adhabu ya asilimia 10. Serikali ilitangaza kufuta utaratibu huo Mei Mosi, mwaka jana.

Vilevile, mwongozo ulielekeza HESLB kukata asilimia moja kwa ajili ada ya uendeshaji kwa mwanafunzi mnufaika, huku marekebisho ya sheria iliyoanzisha HESLB yaliyofanywa na Bunge mwaka 2016, yakisababisha kupanda kwa kiwango cha makato ya kila mwezi kwenye mshahara wa mnufaika kutoka asilimia nane (8) ya awali hadi asilimia 15, mambo ambayo bado yanalalamikiwa na wadau.

Nipashe tunaipongeza serikali kwa kusikia kilio cha wadau wa elimu na kufuta ongezeko la asilimia sita ya mkopo kila mwaka na penalti ya asilimia 10 ya mkopo. Hata hivyo, tunaona sauti za wadau dhidi ya hoja mbili zilizobaki yaani tozo ya asilimia moja kwa ajili ya kupata fedha za kuendesha bodi na kupandishwa kwa kiwango cha makato katika urejeshaji kutoka asilimia nane hadi 15, zina mashiko.

Tunaona kuna haja suala hilo kuangaliwa kwa 'jicho la tatu', ikizingatiwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika ripoti yake ya ukaguzi kwa 2019/20, anabainisha kuwapo shida katika utaratibu huo wa kutoza wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu, huku kukibainika ukiukwaji wa kanuni katika ulipaji wa mishahara ya watumishi.

CAG katika ripoti yake, anarejea utaratibu wa kisheria katika urejeshwaji wa madeni kupitia Mwongozo wenye Kumb. Na. 26/46/01/1/66 wa Novemba 28 mwaka 2012, unaotaka watumishi kulipwa si chini ya theluthi moja ya mishahara yao ya kila mwezi.


Katika ripoti yake, CAG amebaini Mamlaka 35 za Serikali za Mitaa zina watumishi 3,038 wanaopokea chini ya theluthi moja 1/3 ya mishahara yao na na wengine walioamua kupata mikopo mingine kwenye taasisi zingine za kifedha, kila mwisho wa mwezi hawapati kiasi chochote cha mshahara, hali hiyo ikichangiwa na ulipaji wa deni la elimu ya juu.

Katika mazingira ya aina hii, ni wazi kwamba ustawi wa watumishi hao katika kupata mahitaji yao muhimu kama vile chakula, mavazi na malazi uko shakani.

Vilevile, ni hali ambayo Nipashe tunaamini kwa watumishi ambao kiasi kikubwa cha mishahara yao kinatumika kulipa deni la mkopo wa elimu ya juu, kinababisha watumishi kutumia muda wa kazi kwa shughuli zao binafsi ili kujipatia kipato cha ziada, hali inayoweza kudumaza utoaji wa huduma kwa jamii.

Nipashe tunafikiri kuna haja serikali kuangalia tena kiwango cha makato ya mkopo wa elimu ya juu ili kupunguza makali kwa watumishi, mkopo usiodhibitiwa unaweza kuathiri utendaji wa watumishi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mabasi yabanwe kuongeza mapato Stendi ya Magufuli

Na Sabato Kasika

**STENDI** ya mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani iliyoko Mbezi Luis, Manispaa ya Ubungo mkoani Dar es Salaam, ilizinduliwa rasmi Februari mwaka jana na aliyekuwa Rais wa Tanzania wakati huo, Hayati Dk. John Magufuli.

Kuzinduliwa kwa stendi hiyo kulikuwa ishara ya kuanza kutumiwa na mabasi yote kupakia na kushusha abiria ambao kila siku wanasafiri kutoka na kuingia jijini Dar es Salaam.

Tangu ilipozinduliwa rasmi hadi sasa, ni zaidi ya mwaka mmoja stendi hiyo imetumika, huku kukiwa na kero kadhaa ambazo kwa namna moja au nyingine zimechangia kuifanya isiingize mapato ya kutosha.

Miongoni mwa kero hizo ni baadhi ya mabasi kutotumia stendi hiyo kupakia abiria, hali ambayo inakosesha stendi mapato ya fedha ambazo zingetumika kuendelea kuiboresha.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Innocent Bashungwa, ameshtuka na kuagiza mabasi yote yashushe na kupakia abiria ndani ya stendi hiyo.

Kwa mujibu wa Waziri Bashungwa, tangu atoe agizo la mabasi yote kushusha na kupakia abiria ndani ya stendi hiyo, mapato yameongezeka kutoka Sh. 500,000 hadi kufikia 1,195,000 kwa siku.

Ongezeko hilo lina maana kwamba stendi hiyo ilikuwa ikipoteza Sh. 695,000 kwa siku kutokana na baadhi ya mabasi kutofuata utaratibu wa kupakia abiria ndani ya stendi.

Nionavyo ni kwamba, ni vyema agizo hilo liendelee kutiliwa mkazo ili stendi iwe na mapato mengi yatakayosaidia kuiboresha, lakini pia wafanyabiashara waliopanga katika majengo ya stendi hiyo wapate wateja wengi.

Siyo siri kwamba, baadhi ya mabasi kutoshusha abiria au kutokupakia ndani ya stendi hiyo kulikuwa kunachangia kuikosesha mapato na kuwakosesha wateja wafanyabiashara ambao ni wapangaji wanaolipa kodi.

> **Tangu ilipozinduliwa rasmi hadi sasa, ni zaidi ya mwaka mmoja stendi hiyo imetumika, huku kukiwa na kero kadhaa ambazo kwa namna moja au nyingine zimechangia kuifanya isiingize mapato ya kutosha.**

Mtindo wa baadhi ya mabasi kutopakia abiria ndani ya stendi hiyo uliifanya ionekane kana kwamba ubunifu wake hauna tija kutokana na mengine kugeuza maeneo ya Urafiki na Shekilango kuwa stendi.

Ninaamini kwamba uamuzi wa serikali uliotolewa na Waziri Bashungwa, utasaidia kuifanya Stendi ya Magufuli kuwa maarufu na kuiongezea mapato kwa kuwa kila basi linalotoka mikoani, linapaswa kuingia kwanza ndani ya stendi hiyo kabla ya kuendelea na safari.

Katika kupakia abiria kwenda mikoani, ninafikiri kuwekwe masharti kwamba hata kama basi limeanza kupakia nje ya stendi hiyo, ni lazima lipite ndani ya stendi kabla ya kuanza safari ya kwenda mikoani au nje ya nchi.

Ninafikiri kuna haja itumike busara katika hilo kutokana na ukweli kwamba, watu wanaishi maeneo mbalimbali ya jiji ambapo wengine wako jirani na kule ambako mabasi yanaegeshwa kusubiri kuanza safari.

Abiria wa maeneo hayo wanaweza kupanda kwenye mabasi huko yaliko na kwenda hadi Stendi ya Magufuli kabla ya kuanza safari, mradi ushuru wa serikali upatikane.

Wakati wa uzinduzi wake mwanzoni mwa mwaka jana, ilibainishwa kuwa stendi hiyo ikikamilika, ina uwezo wa kuhudumia mabasi ya abiria 1,000, teksi 280 kwa siku, maeneo ya bodaboda, bajaji, mamalishe na babalishe ambao nao wanahitaji kuwahudumia abiria.

Kwa mantiki hiyo, ninaamini kwamba suala la mabasi yote kuingia ndani ya stendi hiyo lina umuhimu wake na halipaswi kubezwa na yeyote.

## Halmashauri zapewa mwezi kupima ardhi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula ametoa, mwezi mmoja kwa halmashauri zote ambazo hazijaidhinisha viwanja vilivyopimwa kupitia fedha za mkopo za mpango wa kupima, kupanga na kumilikisha ardhi, kuhakikisha zinaidhinisha viwanja mara moja na kuanza urejeshaji wa mikopo.

Amesema kwa halmashauri zitakazoshindwa kufanya hivyo, ataiomba Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuingilia kati ili fedha hizo zirejeshwe ndani ya mkataba.

Dk. Mabula alitoa agizo hilo jana aliposhuhudia utiaji saini kwenye mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 4.1 kwa ajili ya Halmashauri nne za Chamwino, Kigamboni, Kishapu na Manispaa ya Lindi ili kupima, kupanga na kumilikisha ardhi.

Alisema kuanzia mwaka 2019/20 hadi mwaka 2021/22, serikali imetoa Sh. bilioni 56.2 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa kupanga, kupima na kumilikisha ambapo hadi sasa halmashauri zaidi ya halmashauri 80 zimepokea fedha hizo lakini nyingi utekelezaji wake upo nje ya mkataba.

Waziri huyo alisema awamu ya kwanza ya mpango huo ilifikia halmashauri 24 mwaka 2019 ambapo iliwezesha kupimwa viwanja zaidi ya 41,733 lakini kati ya fedha zilizotolewa zilizorejeshwa ni Sh. bilioni 4.5 na ambazo hazijarejeshwa ni Sh. bilioni 1.7.

Alisema awamu ya pili ya mpango huo ilishirikisha halmashauri 23 na vyuo vya ardhi, Sh. bilioni 42.3 zikitumika.

"Nitoe tu salamu kwa TAMISEMI mtusaidie sana katika halmashauri kwa kuwa lengo la serikali ni jema lakini umakini haupo, wanapopata pengine wanafikiri ni sadaka imetolewa... Fedha wamepewa tangu Desemba 2021 walikuwa na malengo mpaka sasa hawajaidhinisha kiwanja hata kimoja, hii inasikitisha, kwamba sioni kama tunaliona ni tatizo kwetu wote," alisema.

Aliweka wazi kuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Ridhiwani Kikwete, atakapozunguka kuangalia fedha zilivyotumika kwa ambazo zitakuwa hazijatumika, zirejeshwe ili kuzipa halmashauri zenye utayari.

Naibu Waziri Kikwete alizikumbusha halmashauri wajibu wa kurejesha fedha hizo ili halmashauri zingine zinufaike na hatimaye nchi nzima iwe imepanga matumizi bora ya ardhi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Ally Makoa, alisema zipo halmashauri zimepima lakini zikashindwa kuweka miundombinu rafiki na hivyo maeneo hayo kugeuka vichaka.

# Ajali yaua watano wakienda msibani

**Na Oscar Assenga,** LUSHOTO

WATU watano wamefariki dunia papo hapo na wengine tisa kujeruhiwa baada ya basi dogo aina Coaster walilokuwa wamepanda, kuacha njia na kupinduka wilayani Lushoto mkoani Tanga juzi.

Akizungumzia tukio hilo jana, Mkuu wa Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga, Kalisti Lazaro, alisema ajali hiyo ilitokea juzi katika Kijiji cha Mbaramo, Tarafa ya Umba wilayani humo.

Alisema gari hilo lilikuwa linarejea Dar es Salaam kutoka Kijiji cha Mbaramo na kwamba abiria waliokuwa ndani ya gari hilo walikuwa wanakwenda msibani.

Inadaiwa kuwa dereva wa gari hilo alishindwa kulimudu kwenye kona hali iliyosababisha gari hilo kupinduka.

Mkuu wa Wilaya alitaja majina ya waliofariki dunia katika ajali hiyo kuwa ni Sebastian Kamwedi (35), Godfrey Martin (70), Jackline Shemela (37), Emanuel Philipo, mtoto wa miezi miwili na Elly Gumbo.

Alisema majeruhi sita wamepelekwa katika Hospital ya Rufani Bombo mkoani Tanga huku watatu wakiwa wanaendelea kupata matibabu katika Kituo cha Afya Mnazi kilichoko wilayani Lushoto.

Lazaro alitoa wito kwa madereva wageni ambao wanaelekea wilayani humo wanapopanda milima ya Usambara, wawe makini ili kuepukana na ajali ambazo zinaweza kuepukika na kuokoa maisha ya watu.



Baadhi ya wanachama wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kipunguni, jijini Dar es Salaam, wakichuma mboga kwenye moja ya bustani zao, jana. Kituo hicho, hutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa watu na vikundi mbalimbali ili kupunguza tatizo la ajira na ukatili unaosababishwa na hali ngumu ya kiuchumi katika jamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia apiga simu na kuagiza ulinzi wananchi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka viongozi wa mikoa kufanya kazi ya kusimamia miradi ya maendeleo huku wakilinda usalama wa wananchi ili Taifa lipate maendeleo haraka.

Alitoa maagizo hayo jana alipozungumza kwa njia ya simu na wananchi wa Mkoa wa Mbeya baada ya kumpigia Mkuu wa Mkoa huo wakati wa hafla maalumu ya kuipongeza serikali kwa utekelezaji wa miradi ndani ya mkoa huo.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo kuendelea kushirikiana na serikali kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na kuhakikisha wanailinda ili idumu.

Pia aliwapongeza viongozi wa Mkoa wa Mbeya pamoja na wananchi wa Mkoa huo kwa kuandaa hafla ya kuipongeza serikali anayoiongoza kutokana na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo.

"Nimepata taarifa kwamba mmeandaa matembezi na mkutano wa kuipongeza serikali, ninawashukuru sana na ninawataka tushirikiane kwenye kazi ili nchi yetu ipate maendeleo kwa haraka, lindeni sana usalama wa wananchi," aliagiza Rais Samia.

Akizungumza kwenye mkutano uliofanyika kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini hapa, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema serikali imetekeleza miradi mingi ya maendeleo ndani ya mkoa huo.

Alisema katika sekta ya elimu serikali kwa kutumia fedha za Mpango wa Maendeleo na Mapambano dhidi ya Ugonjwa wa UVIKO-19, imejenga vyumba vya madarasa kwenye shule mbalimbali za sekondari zikiwamo shule shikizi.

Alisema mbali na shule hizo pia serikali imejenga maabara kwenye shule mbalimbali za sekondari, ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye vyuo pamoja na ukarabati wa shule kongwe ikiwamo Shule ya Sekondari Rungwe.

Vilevile, alisema serikali imejenga miradi mbalimbali ya maji kwenye maeneo yaliyokuwa na matatizo ya maji ukiwamo Mradi wa Maji wa Shongo ambao umegharimu Sh. bilioni 3.5 ambao umemaliza tatizo la ukosefu wa maji katika Mji wa Mbalizi.

"Lakini pia serikali imeahidi kuipanua barabara yetu Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) kuanzia Uyole mpaka Songwe kwa kuifanya kuwa ya njia nne, hii itatusaidia kupunguza msongamano wa magari hapa katikati ya mji," alisema Homera.

Katibu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa, Kenan Kihongosi, aliupongeza uongozi wa Mkoa wa Mbeya kwa kuandaa mkutano huo wa kuipongeza serikali na Rais Samia kwa utekelezaji wa miradi huku akisisitiza kuwa vijana ni miongoni mwa makundi yanayonufaika.

Matembezi hayo yalihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, dini, mila na wananchi ambapo kabla ya kufanya mkutano kwenye Uwanja wa Sokoine, walishiriki matembezi maalum umbali wa zaidi ya kilomita tano.

MAKALA

# Migogoro ya ndoa inachangia magonjwa ya akili

NDOA ni zawadi ya Mungu kwa mwanadamu na kitovu cha familia, jamii, taifa na malezi. Mungu alianzisha taasisi hii ya ndoa ili watu waingie, waipende na kuifurahia kwa kuwa ndoa ni taasisi ya heri, si taasisi ya vita na machinjio ya watu.

Ni mpango asilia wa Mungu kwamba mume na mke waishi pamoja katika amani na utulivu kamili. Amani ni moja ya matunda ya haki na zawadi kutoka kwa Mungu inayomwajibisha binadamu.

Amani ni msingi wa wema, heshima na maendeleo endelevu na fungani ya binadamu. Hivyo, amani ni zawadi inayopaswa kutunzwa kwa njia ya kuwa na ndoa imara na malezi yenye dhamira nyofu kwa kulinda na kuheshimu utu wa binadamu, ustawi na maendeleo ya familia, jamii na taifa. Mume na mke katika ndoa ni watu wanaotegemeana. Mungu aliumba mwanamume na mwanamke ili wahitajiane na kutegemeana katika maisha; wafurahi na kufurahishana.



### MIGOGORO YA NDOA

Pamoja na kusudi jema la Mungu la kuanzisha taasisi ya ndoa, wanadamu wameharibu misingi na ladha ya ndoa. Hali hii inapotosha kwa kiasi kikubwa kusudi na maana halisi ya taasisi hii takatifu. Kwa baadhi ya familia, ndoa imegeuka kuwa jela ya nyumbani. Migogoro ya mara kwa mara isiyo na ukomo imekuwa mtindo wa maisha.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2022/23 ya wizara yake, pamoja na mambo mengine, alibainisha kuwa hadi kufikia mwezi Aprili, 2022, wizara imepokea jumla ya migorogo ya ndoa 39,571 ambapo migogoro 19,262 ilipata suluhu, migogoro 15,718 bado iko katika usuluhishi, huku migogoro 4576 ikiwa iko mahakamani. Hii inaonesha dhahiri kuwa migogoro ya ndoa nchini ni janga la taifa.

Kimsingi, migogoro ya ndoa hujeruhi nafsi, huondoa hisia za mapenzi na mvuto miongoni mwa wanandoa. Hali hii huchangia matatizo ya afya ya akili kwa sababu ya msongo mkubwa wa mawazo. Magonjwa ya akili ni kichocheo cha watu kufanya vitendo vya ukatili na mauaji miongoni mwa wanandoa.

Moja ya matukio ya kusikitisha ni tukio lililotokea mwezi Mei 28, mwaka huu huko Busweru katika Mkoa wa Mwanza ambapo binti wa miaka 28 aliuawa na mumewe kwa kupigwa risasi kwa madai ya wivu wa mapenzi. Baadaye mumewe naye alidaiwa kujiua kwa kujipiga risasi.

Mbali na tukio hilo, huko mkoani Shinyanga mwanamke anadaiwa kumjeruhi mumewe kwa kumkata sehemu za faragha kwa tuhuma za usaliti. Huko Tunduru mkoani Ruvuma mwanamke amefariki na kuacha mtoto wa miezi 11 kwa kile kinachodaiwa kuwa ameuawa kwa kupigwa risasi kichwani na mchumba wake kutokana na wivu wa mapenzi.

Huko Butiama mkoani Mara, mwanamke mwingine alidaiwa kumuua mumewe kwa kumchoma na kitu chenye ncha kali kwa tuhuma hizo hizo za usaliti. Hali kadhalika, Serengeti mkoani Mara ilitolewa taarifa na Jeshi la Polisi ya mume kudaiwa kumjeruhi mkewe kwa kumwingiza panga sehemu za siri, akimtuhumu kuwa na uhusiano na mwanamume mwingine.

Huko mkoani Ruvuma, Jeshi la Polisi limetoa taarifa ya mwanamke aliyemjeruhi mumewe kwa kumkata na wembe sehemu za siri akiwa usingizini na kumsababishia maumivu makali. Matukio ya namna hii bado yanaendelea kujitokeza mara kwa mara katika jamii.

Ni muhimu ifahamike kuwa, matukio haya yanapotokea katika jamii hayaathiri wanandoa pekee, bali na watoto waliozaliwa katika ndoa hizo kwani mfumo wao wa maisha unavurugwa.

Halikadhalika, wazazi na familia wanazotoka wanandoa huathirika pia kwani hakuna mzazi ambaye angependa kuona mtoto wake anapata matatizo. Taifa nalo linakuwa linapoteza nguvu kazi yake muhimu. Hatua za makusudi zinahitajika kuchukuliwa kwa maslahi mapana ya familia, jamii na taifa kwa ujumla.

### MAGONJWA YA AKILI

Kabla ya kueleza nini kifanyike ili kukabiliana na tatizo hili, ni muhimu kwanza kufahamu maana ya magonjwa ya akili, sababu zake na hali ilivyo duniani na katika jamii yetu.

Kwa mujibu wa maelezo ya kitaalamu kutoka Kituo cha Afya -Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, magonjwa ya akili ni matatizo ya ubongo ambayo humfanya mtu kuwa na hisia, fikra, na matendo tofauti na yale yanayotarajiwa na jamii na kushindwa kukabiliana na shida za maisha.

Magonjwa ya akili yanaweza kusababishwa na sababu za kibailojia au kisaikolojia kama vile kurithi vinasaba kutoka kwa wazazi, magonjwa ya muda mrefu, matumizi ya dawa za kulevya, uvutaji bangi na ulevi wa pombe kwa sababu madhara yake huenda moja kwa moja kwenye ubongo; na migogoro ya mara kwa mara isiyokoma.

Sababu zingine ni pamoja na vitendo vya ubakaji, unyanyasaji, ukatili wa nyumbani (domestic violence), msongo wa mawazo wa muda mrefu, ugumu wa maisha kama vile majanga, kukosa au kupoteza ajira.

Kwa upande wa watoto, unyanyasaji wa kingono, kukosa matunzo stahiki, ugomvi wa mara kwa mara wa wazazi wao, kutokuthaminiwa na kutelekezwa huwaathiri sana watoto kisaikolojia na kusababisha matatizo ya afya ya akili wangali wadogo.

Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonesha kwamba, takribani asilimia 20 ya watoto na vijana duniani wana matatizo ya afya ya akili.

### HALI ILIVYO

Kwa mujibu wa takwimu za WHO za hadi mwaka 2022, takribani watu bilioni moja duniani wanaishi wakiwa na magonjwa ya akili (mental disorders), ambapo kati ya watu wanne (4) mmoja ana tatizo la afya ya akili. Takwimu hizo pia zinaonesha kwamba asilimia 75 ya watu wenye matatizo hayo hawapati matibabu kila mwaka.

Taarifa ya Meneja wa Mpango wa Taifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya Dk. Omary Ubuguyu, kama alivyonukuliwa katika magazeti ya Tanzania Oktoba 5 mwaka jana, inabainisha kuwa, idadi ya wagonjwa wa akili imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka.

Mwaka 2018 kulikuwa na wagonjwa 357,799, mwaka 2019 walikuwa wagonjwa 380,000 na mwaka 2020 walifika wagonjwa zaidi ya 500,000.

Hizi ni takwimu za wagonjwa waliofika hospitalini kupatiwa matibabu. Inawezekana wenye matatizo haya ni wengi katika jamii kwa sababu ya uelewa mdogo wa watu wengi kuhusu magonjwa ya akili.

Dalili magonjwa ya akili

Dalili za magonjwa ya akili (kwa kutaja kwa uchache) ni pamoja na wivu uliopitiliza, kuhisi maisha kutokuwa na thamani na mtu kutamani kufa au kuua kuliko kuishi; kuwa na woga na wasiwasi kupita kiasi; kuongea au kutokuongea kupita kiasi; hasira kali za haraka; mtu kujitenga na wenzake na kupenda kukaa mwenyewe muda mwingi; kutokujijali kwa usafi na mwonekano wa nje; kukosa usingizi au kulala usingizi sana kupita kiasi; kusahausahau vitu na kupoteza kumbukumbu; kuwa na imani zisizo za kawaida, na mawazo kukosa mtiririko unaoeleweka.

### NINI KIFANYIKE?

Migogoro ya ndoa inahitaji kupatiwa ufumbuzi mapema ili kuwaepusha wanandoa na athari zitokanazo na migogoro. Ni muhimu watu wajenge utamaduni wa kupima afya ya akili kabla ya ndoa kwa sababu wako baadhi ya watu wamezaliwa wakiwa na matatizo ya afya ya akili.

kwa vitendo vya ukatili na mauaji ya wanandoa katika familia ni kiashiria kuwa, baadhi ya watu wameoa au kuolewa na watu wenye matatizo ya afya ya akili.

Elimu kwa umma kuhusu masuala ya afya ya akili inabidi kutolewa ili kuwasaidia wananchi kujitambua kwani watu wengi bado hawana ufahamu wa kutosha kuhusu tatizo hili. Matokeo yake watu hawaoni umuhimu wa kupima na kujua hali zao za afya.

### TAASISI YA NDOA

Taasisi ya ndoa ni taasisi nyeti yenye misingi, kanuni, sera, taratibu na miiko yake. Ni muhimu watu watamani na kudhamiria kujifunza kwa lengo la kuifahamu vizuri taasisi hii kabla ya ndoa ili kuepuka matatizo yasiyo ya lazima.

Watu wengi wameoa au kuolewa pasipo kuwa na ufahamu na maarifa ya kutosha kuhusu taasisi ya ndoa matokeo yake wamekuwa vivuruge. Nguvu kubwa huelekezwa katika kuandaa sherehe za harusi na siyo kujiandaa kuwa mume na mke bora.

### UHUSIANO NA MUNGU

Suala la usalama katika ndoa ni jambo muhimu. wanandoa wafahamu kwamba, hakuna usalama katika ndoa Mungu asipohusika. Hivyo, wanandoa wawe na uhusiano mzuri na Mungu na wao kwa wao ili wawe salama.

Kutokuwa na uhusiano mzuri na Mungu kunawaondolea wanandoa kinga ya kiroho na hofu ya Mungu ndani yao. Kinachobaki kati yao ni kuumizana na kukosa roho ya msamaha.

Kuomba msamaha

Ndoa ni safari ya maisha ambapo kuna kukosea na kukosana njiani. Ni muhimu wanandoa wawe wepesi kujifunza, kujikosoa, kujisahihisha na kuombana msamaha pale mtu anapohisi kumkosea mwenzake. Ni vema ifahamike kuwa, hakuna ndoa yenye afya njema bila zoezi la msamaha. Msamaha ni dawa ya furaha ya familia.

Msamaha ni muhimu kwa afya yetu ya kihisia na kuendelea kuishi kwa heri. Asiyeomba msamaha na asiyesamehe hana amani katika nafsi yake na hawezi kuwa na ushirika na Mungu. Pia, mtu wa aina hiyo hawezi kuwa na uhusiano mwema na binadamu mwenzake.

Watu wasioomba msamaha na wasiosamehe ni wagonjwa wa kimwili, kihisia na kiroho. Siku zote huteseka na kuishi kwa vinyongo na roho ya visasi na maangamizi. Bila msamaha, familia inakuwa uwanja wa migogoro, ngome ya uovu na maafa.

Migogoro ya ndoa ni adui wa maendeleo kwani maendeleo na ustawi wa familia na taifa unategemea ndoa imara. Kwa hiyo, ni muhimu kila mwanandoa ajiheshimu, atambue nafasi, wajibu na mipaka yake katika ndoa ili kuifanya ndoa kuwa baraka.

[Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na

# MAISHA

JUNI 12, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 13

**Mbwembwe za vijora**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Hivi ndivyo unapaswa kusafisha sofa



Ukurasa 12

**HARUSI**




**NYWELE ZENYE AFYA**


# Njia hizi hutibu kukatika nywele

Ukurasa 14

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | P | A | N | G | A |
| ■ | U | ■ | ■ | A | ■ |
| O | N | A | ■ | N | ■ |
| ■ | G | ■ | O | G | A |
| ■ | U | ■ | ■ | W | ■ |
| P | A | N | D | E | ■ |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI




## FUMBO TOTO

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | | | | | |
| ■ | | ■ | ■ | | ■ |
| | | | ■ | | ■ |
| ■ | | ■ | | | |
| ■ | | ■ | ■ | | ■ |
| | | | | | ■ |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UDA, MKE, TAMKA, TENGA, GANDIA, TAKASA

## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Grace alikuwa chumbani kwake akijisomea vitabu kwa muda mrefu. Aliamua kutumia muda huo kujikumbusha masomo yake kutokana na siku chache zinazokuja kuna mtihani wa kumaliza muhula.

Wakati akiendelea kusoma, mama yake aliingia chumbani na kumtaka aende sebuleni ili akale chakula.

**Mama:** Mwanangu nenda sebuleni ukale chakula na wenzako

**Grace:** Mama siwezi kula kwa sasa kwa sababu najiandaa na mtihani.

**Mama:** Lakini kujiandaa bila kula? Ebu nenda mwanangu!

**Grace:** Mwalimu alituambia kwamba 'Penye udhia pana zarubia' najitahidi kutafuta maana yake.

**Mama:** Mwalimu wako alimaanisha kila penye matatizo kuna faraja baadae na si vinginevyo.

**SWALI**

Kilimo cha pamba kinapatikana mikoa gani ya Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Fedha haipendi kutumiwa bali inataka kuongezwa!

***KARIBU tena msomaji tuendelee kujadili siri iliyojificha kwenye fedha. Wiki iliyopita nilitaja siri mbili, huku nikisisitiza kwamba fedha kama fedha haina thamani yoyote mpaka iambatane na bidhaa. Fedha huenda pale ilipo bidhaa.***

Leo tuangalie siri ya tatu ya fedha. Ili uende kupata fedha zaidi zingatia ukweli huu kwamba fedha siyo kwa ajili ya matumizi bali kwa ajili ya kuwekeza. Kwa kadri unavyopunguza matumizi na kuongeza uwekezaji, ndivyo utakavyoongeza fedha zako. Ukizingatia kununi hii utashangaa kuona matumizi yako mengi hayakuwa ya lazima.

Wengi wetu hatujui uwekezaji sahihi wa fedha na matokeo yake tunageuka kuwa watumwa wa fedha. Unaamka saa kumi usiku na kukimbizana na fedha mpaka saa tatu usiku kila siku.

Wengine wamehama na kuacha familia na kwenda mbali kutafuta fedha. Linalotokea kwa sababu ya kukosa ufahamu wa siri ya fedha, unaingia kwenye matumizi makubwa ya fedha na mwisho wa siku zinakukimbia.

Kwa mfano, umeacha familia yako ukaenda mbali kutafuta fedha. Pengine umefanikiwa kuipata kwa shughuli au biashara unayofanya. Lakini ukaingiwa tamaa na kuanza kupepesa macho kutafuta uhusiano nje ya ndoa yako!

Utajidanganya kwamba unajiliwaza kwa muda, lakini watu wengi walioingia kwenye mtego wa aina hiyo wamejikuta wakizama na wakipoteza mweleke, hivyo kuanza kutumia fedha nje ya malengo. Badala ya kuongezeka zinaanza kupungua kwa sababu amewekeza sehemu ambayo siyo sahihi.

Kumbe! Ameangukia mikononi mwa wafyonza fedha na siyo waongeza mitaji. Ndio maana nikasema kwamba fedha haipendi kutumiwa, inataka kuongezwa na ndipo yule aliyeijua siri hii ataona fedha zake zikiongezeka kila wakati bila mahangaiko mengi.

Mtu asiyejua siri hii, fedha zitakuwa zinamkimbia na mwishowe hata kile alicho nacho huondoka. Hata Mungu anasema katika neno lake kwamba, “Kwa maana yeye mwenye kitu atapewa, naye atazidishiwa tele; lakini yeye asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang’anywa”.

Fedha kama ilivyo tabia ya maji haipandi kilima bali hufuata mteremko. Unapokiuka kanuni hii unajikuta unapata fedha kidogo kwa mahangaiko mengi hadi kufikiria una laana au umelogwa.

Wapo watu wanaoamini kwamba wakipata mtaji wa kutosha wataweza kufanya biashara ya mafanikio. Mnaweza watu wawili mkapata mtaji wa silingi milioni kumi kila mmoja na kuamini kwamba hizi zinatosha kukupa mafanikio.

Baada ya mwaka, mmoja kati ya wale wawili atakuwa ameajiriwa na mwenzake. Shida ni nini wakati wote walipatiwa mtaji sawa? Fedha siyo kwa matumizi bali kwa uwekezaji. Ni kwa nini unapokuwa na mbegu huzitumii bali unakwenda kuzipanda.

Ukimpa mkulima kilo hamsini za mahindi ili akapande halafu akaenda kuzisaga kupata unga, utamuelewaje? Wengi wetu tunapopata fedha, wazo la kwanza na lenye nguvu ni jinsi ya kuzitumia. Mara nyingine matumizi yenyewe ni ‘halali’ kabisa! Yaani tuna roho ya kula mbegu na wakati huo huo tunatarajia mavuno.

Fedha ina hulka ya ajabu kabisa. Ina uwezo wa kutambua mtizamo wako. Kama akili yako imeelekea sana katika matumizi, fedha itakuletea matumizi ya kila aina, tena matumizi ya kawaida kabisa.

Mfano, magonjwa, misiba, shida toka kwa ndugu na kadhalika. Vyote hivi hutokea wakati una fedha. Vikiisha, zile shida haziji tena hadi pale utakapokuwa na fedha zingine.

Ifahamike kwamba mwenye mawazo ya kuwekeza, fedha nayo inamtambua. Anapopata fedha, fursa za kuwekeza hujitokeza. Utatafutwa ili ununue mashine, shamba, nyumba au hisa kwenye makampuni.

Dunia nzima hivi sasa ni uwekezaji, hivyo na sisi katika ngazi ya mtu mmoja mmoja akili zetu yafaa zifunguke sote tuzingatie umuhimu wa kuwekeza.

Ili ufanye uwekezaji wa tija kwenye kilimo, ufugaji, tehema, sanaa na kadhalika, chukua muda wa kujielimisha katika eneo unalotaka kufanyia biashara. Fanya utafiti wa kina ili upate picha halisi ya biashara unayotaka kufanya.

***Wiki ijayo nitakupa siri ya nne kubwa itakayokusaidia kuagana kabisa na umasikini. Bila shaka umejifunza mengi hadi saa kuhusu siri ya fedha. Endelea kufuatilia makala hizi kwa mafanikio ya uchumi wa familia yako. Je, una maoni au kisa? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Hili la pikipiki lituamshe kumaliza urasimu

APRILI 4 mwaka huu, Rais Samia Suluhu aligawa pikipiki na vitendea kazi vingine kwa maofisa ugani wa kilimo nchini kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi na kuongeza huduma kwa wakulima.

Katika hafla hiyo maalum, jumla ya pikipiki 6,700 zilitolewa, Rais Samia akiridhia baada ya miaka miwili ziwe mali yao, ili wazitunze na zidumu kwa muda mrefu.

Kwa sasa ni miezi miwili imepita lakini vifaa hivyo havijawafikia wahusika, badala yake zimehifadhiwa kwenye ofisi za umma, jambo ambalo linazua maswali mengi.

Mathalani, karibu kabisa na ukumbi wa Bunge Dodoma lango la 56 kuna majengo yanatumiwa na idara za Wizara ya Kilimo, kuna pikipiki nyingi zimeegeshwa zikipigwa na jua na mvua usiku na mchana.

Pikipiki hizo zitaanza kuharibika kabla ya kuwafikia maofisa ugani kwa kuwa zinanyeshewa na mvua, zinapigwa na jua usiku na mchana, maana yake hadi inamfikia mhusika imeshakuwa na matatizo fulani.

Wizara ya Kilimo ilieleza lengo la kuwa na vitendea kazi hivyo ni kuleta mapinduzi ya kilimo, lakini hadi sasa hakuna ufafanuzi wa kina kwa nini pikipiki hizo zimeendelea kuegeshwa maeneo tofauti tofauti pasipo kuwafikia wahusika.

Juni 8 mwaka huu, wakati wa maswali bungeni, Mbunge wa Viti Maalum, Khadija Aboud, katika swali la nyongeza alitaka kujua lini serikali itaanza kugawa pikipiki hizo.

Alisema serikali imenunua pikipiki kwa maofisa ugani lakini hazijagawanywa, mbunge huyo akieleza hofu yake ya uchakavu na kuchelewesha kuwahudumia wakulima.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alisema bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/23 na hasa eneo la huduma za ugani imeongezeka kutoka Sh. milioni 600 hadi Sh. bilioni 500 kwa miaka miwili na kazi kubwa ni kununua pikipiki hizo.

Alisema kulikuwa na taratibu za ndani za kufuata ambazo zimekamilika na kunzia Juni 7 mwaka huu, ugawaji wa pikipiki ulianza kwa Dodoma zilipelekwa 264 na Singida 161, watafuatiwa na Tabora na baadaye mikoa mingine.

Saa chache baadaye, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alizuru maeneo zilikowekwa pikipiki hizo na kutoa siku tano pikipiki zote ziwe zimegawanywa kwa maofisa ugani, huku akisema sababu iliyoelezwa kuwa hazina namba za usajili haina msingi.

Siku iliyofuata tuliona zikiondolewa zilikokuwa zimekusanywa na baadhi ya wakurugenzi wakizikabidhi kwa maofisa ugani, jambo lililofanya nijiulize walisubiri maelekezo ya kiongozi wa juu ndipo wazigawanye au utaratibu urahisishwe?

Kimsingi, ninakubaliana na serikali kuwa kulikuwa na taratibu za kufuata, lakini lipo jambo la kujifunza kuwa huenda taratibu zilizopo zina urasimu kiasi cha kukwamisha nia njema iliyopo, lakini watu hao hao wanaweza kuzirahisisha ili kazi ziende kwa kasi.

Kama miezi miwili itatumika kukamilisha taratibu ndani ya wizara, ni wazi katika ngazi ya mikoa, wilaya, tarafa, kata hadi vijiji itachukua mara mbili ya muda huo.

Ni nini kilikwamisha taratibu hizo kukamilika kabla ya hafla ya kitaifa ya kugawa vifaa hivyo ili wiki moja baadaye iwe ni kuzisafirisha kwenda kwa wahusika ngazi ya kata na vijiji?

Tuna mikoa na wilaya ambazo mtu analazimika kusafiri saa nyingi ili kufika. Mathalani, Kigoma, Mbulu, Dongobeshi, Nyasa, Loliondo, Kagera, japo kutaja kwa uchache. Maana yake vifaa hivyo vitachukua muda mrefu na vitaendelea kuharibika kwa sababu ya muda na huenda hadi wengine wanakabidhiwa itachukua miezi sita.

Kwa taratibu hizo hizo zitakapofikishwa kwenye halmashauri ambako ndiko maofisa ugani wanawajibika moja kwa moja, wakurugenzi wa halmashauri watafuata taratibu zilizopo hadi kugawa vifaa hivyo.

Ipo mikoa ya jirani na Bandari ya Dar es Salaam ambayo huenda ilitumika kuingiza mzigo huo, sitaki kuamini kwamba zote zili- letwa Dodoma ndiyo zirudishwe mikoa ya Morogoro, Pwani, Lindi, Mtwara na Songea ambako kwa kutokea Dar huenda ni karibu zaidi na gharama ni ndogo.

Kama hali itaendelea kuwa hivi, tutarajie zitatengwa fedha nyingine za ukarabati au atakayekabidhiwa ataitumia baada ya muda mfupi itaanza kusumbua na kuhitaji matengenezo au wakati anakabidhiwa baadhi ya matairi yameshapasuka au kuharibika kwa namna yoyote ile.

Vifaa hivi havijatengenezwa nchini, maana yake vilisafirishwa kwa muda mrefu vilikaa kwenye meli baharini kisha kuletwa Dodoma, na sasa imepita miezi miwili ndiyo serikali inaanza kugawa

Lazima kuangalia taratibu zinazotengeneza mazingira magumu au ya hasara zikarahisishwa ili kuepusha usumbufu wa namna yoyote ile, fedha iliyotumika kununua vifaa hivyo ni ya umma, kama kutakuwa na matengenezo itatumika fedha nyingine ya umma.

Hii ni hasara kwa Watanzania ambayo kwa namna yoyote ile inapaswa kuepushwa kwa kurahisisha taratibu za ndani, na kukabidhi vifaa hivyo kwa maofisa ugani ili wananchi waone faida yake.

Ipo mikoa kipindi hiki ni msimu wa kilimo au mavuno au palizi na wangehitaji huduma za ugani kwa karibu, lakizi haziwafikii kwa sababu hakuna vitendea kazi.

Lakini wapo wanaofuga wanahitaji huduma za ugani, kilio kikubwa ni wakulima na wafugaji kufikiwa na huduma hizo na sababu kubwa ilikuwa ni kukosekana usafiri kwa kuwa halmashauri nyingi hazina vyombo vya usafiri vya kutosha.

Hali hii imeonekana kwenye pikipiki, lakini taratibu kama hizi zinatokea maeneo mengine na kukwamisha shughuli za serikali au kuchelewesha huduma kwa wananchi. Ni lazima kuchukua hatua kurekebisha taratibu zenye urasimu au kama ni uzembe wa wachache hatua zichukuliwe.

# HARUSI












Ilikuwa furaha ya kipekee baada ya Clinton Chitalilo kufunga ndoa na Hilda Mwaimu Juni 4 mwaka huu katika kanisa la Sabato Ilazo jijini Dodoma, kisha sherehe ya aina yake ya kuwapongeza ilifanyika siku ya pili yake katika ukumbi wa Four Hotel iliyopo Kisasa.

## MITINDO



# Mbwembwe za vijora

VAZI aina ya vijora limekuwa maarufu miongoni mwa wanawake kutokana kuhusishwa na mambo mbalimbali ya kijamii katika mitaa ya uswahilini.

Vijora huvaliwa kwa wingi katika sherehe mbalimbali kama sare za harusi, unyago na kuwatoa watoto. Pia hutumika kama vazi la kawaida la nyumbani.

Hata hivyo, vazi hilo licha ya kupata sifa zenye utata, lakini ni nguo nzuri na yenye heshima kama ikivaliwa vizuri.

Katika kulijengea heshima vazi hilo, Baadhi ya wabunifu wameongeza vionjo kwa kutengeneza mitindo mbalimbali ya kisasa zaidi ambayo imesababisha watu kupagawa.

Unapovaa kijora inapendeza zaidi kuambatana na mtandio kichwani wa rangi moja na mguuni ni vyema ukavaa viatu vya wazi.

UREMBO



NYWELE ZENYE AFYA

# Njia hizi hutibu kukatika nywele

KUPOTEZA nywele ni hali ya kawaida, ingawa inaweza kusababishwa na matatizo ya afya yako. Hivyo huleta athari kisaikolojia kwa baadhi ya watu.

Tatizo hilo husababishwa na mambo yafuatayo, kimaumbile, usawa wa homoni, hali ya vimelea vya ngozi ya kichwa, kukaza nywele na utapiamlo.

**Njia ya kutunza**

Kuna dawa za asili ambazo unaweza kutumia kukuza nywele zako kwa asili.

Kadhalika kusugua ngozi ya kichwa, ambayo inaweza kutumika na mafuta ya nywele na maski, hufufua ngozi ya kichwa na inaweza kuboresha nywele.

Kutumia mafuta ya Alovera kutibu tatizo ambayo husaidia kupunguza ngozi ya kichwa na unyevu wa nywele.

Inaweza kupunguza mba na kufungua vinyweleo vinavyoweza kuziba kwa mafuta ya ziada.

**Mafuta ya Nazi**

Mafuta ya nazi yana asidi mbayo hupenya shimo la nywele na kupunguza upotezaji wa protini kutoka kwa nywele.

**Mafuta ya samaki**

Kuna asidi ya mafuta ya omega inaweza kusaidia kuboresha nywele zako kutoka kwenye mizizi, kwa kuwa zimejaa virutubisho na protini.

Kuchukua nyongeza ya omega, pamoja na antioxidants, husaidia kuboresha nywele na pia hupunguza kupoteza nywele.

**Juisi ya vitunguu**

Ikiwa unaweza kumudu harufu ya juisi ya vitunguu, unaweza kupata faida zake za thamani yake.

Ni chanzo cha kuaminika cha kukuza ukuaji wa nywele na kutibu alopecia areata.

**Mafuta ya musk**

Ni mmea wenye harufu nzuri. Unaweza kutumia mafuta ya musk kukuza ukuaji wa nywele na kuchochea mzunguko wa damu.

**Limao**

Unaweza kutumia maji safi ya limao au mafuta ya limao, kwani zote zimethibitishwa kuongeza ubora wa nywele na ukuaji.

Mafuta ya limao yanaweza kukusaidia kudumisha afya ya ngozi ya kichwa na kuchochea ukuaji wake.





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Jiburudishe na kachori

KACHORI ni chakula kitamu ambacho unaweza kula wakati wowote unapojisikia.

Kachori hazina kazi kubwa katika kutengeneza ingawa unahitajika kuwa na muda wa kutosha katika kuandaa chakula hiki.

**Mahitaji**

Viazi mbatata vinne vya wastani, nyama ya kusaga kikombe kimoja cha chai, kitunguu kimoja cha wastani na karoti moja, pilipili hoho nusu, kitunguu swaumu, tangawizi, binzari nyembamba nusu kijiko cha chai



na binzari manjano nusu kijiko cha chai.

Kadhalika curry powder nusu kijiko cha chai, limao nusu kipande, pilipili ya unga nusu kijiko cha chai

Giligilani, chumvi, mafuta na unga wa ngano kiasi.

**Matayarisho**

Katakata vitunguu na hoho



katika vipande vidogo vidogo na kisha kwangua karoti na uweke pembeni. Chemsha viazi na chumvi kidogo vikiiva viponde na uviweke pembeni.

Baada ya hapo tia nyama limao, chumvi, kitunguu swaumu na tangawizi ichemshe mpaka iive na uhakikishe maji yote yamekauka.

Kisha tia binzari zote, pilipili, curry powder, giligilani, vitunguu, hoho na karoti. Pika mchanganyiko huo kwa muda wa dakika 3 na kisha ipua.

Baada ya hapo changanya na viazi kisha tengeneza maduara ya kiazi na uyaweke pembeni. Chukua unga wa ngano kiasi na uchanganye na maji kupata uji usiokuwa mzito au mwepesi sana, baada ya hapo chovya madonge katika huo uji na uyachome katika mafuta.

Hakikisha zinaiva na kuwa rangi ya brown na hapo zitakuwa tayari kwa kuliwa.Unaweza ukazisevu na chatney yoyote unayopendelea.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Hivi ndivyo unapaswa kusafisha sofa

WASWAHILI husema 'umaridadi huficha umaskini'. Leo ninataka tuangalie umaridadi katika usafi wa sofa kwa sababu hili nalo ni kiungo muhimu cha kung`arisha na kuleta mvuto ndani ya nyumba.

Kama ilivyo katika usafi wa mambo mengine kwenye nyumba, sofa inahitaji usafi, tena kwa umaridadi wa hali ya juu hususani kwa nyumba zenye familia kubwa.

Baadhi huwa hatuna utaratibu wa kusafisha sofa zetu mara kwa mara, huenda ni kutokujua zinatakiwa kusafishwa au kutokujua vitu vinavyotumika katika kusafishia na mahali pa kuvipata.

Sofa zikifutwa kawaida au kwa kutumia maji matokeo yake huwa sio mazuri kwa kuwa badala ya kung`ara huanza kuchafuka na kuchakaa zaidi.



Kwa wale wanaomiliki sofa za vitambaa, wanatakiwa kutumia njia sahihi zaidi ya kusafisha badala ya kufuta kienyeji ili kuzitunza zisiharibike kwa sababu kitambaa kiko katika hatari zaidi ya kuharibika endapo utaratibu mzuri hautafuatwa wakati wa kusafisha.

Yapo maji maalum au kwa lugha nyingine 'spray' inayotumika kusafishia sofa hizo, ni vyema ukaitafuta hiyo kwa sababu inapatikana kwa wingi madukani.

Lakini kabla ya kuanza kutumia, hakikisha sofa zako zimepanguswa na kutolewa vumbi lililokuwa limeng`ang`ania kwa kutumia kifaa maalum cha kupuliza vumbi ama kwa kutumia kitambaa safi.

Baada ya kuhakikisha umesafisha kila kona, ndipo unatakiwa kuanza kupulizia.

Kwa kuzingatia ujazo katika chupa hizo maalum za maji ya kusafishia sofa, unaweza kutambua utumie chupa ngapi na kwa sofa ngapi hasa kulingana na ukubwa wa tatizo japokuwa ninaamini moja inaweza kutosha labda kama sofa imechafuka kupitiliza.

Unachopaswa kufanya ni kupulizia katika sehemu ndogo ili wakati huo huo uwe unafuta na kitambaa kisafi na unatakiwa kufanya hivyo mpaka umalize.

Baada ya kumaliza kazi hiyo katika maeneo yote, unaweza kuliacha likauke na hapo ndipo utaanza kuona matokeo mazuri kwa sababu mng`ao wa rangi yake utakuwa mzuri zaidi.

Kumbuka kwamba kufanya usafi huo katika sofa hauhitaji gharama kubwa sana endapo utafanya mwenyewe, labda uamue kutumia gharama kubwa kwa matakwa yako kwa kutumia wataalamu wa kukodi.

Pia kadri utakavyojenga utaratibu wa kupenda kusafisha sofa mara kwa mara ndivyo hivyo gharama itazidi kuwa ndogo kwa sababu hututumia spray nyingi kama ambavyo utasafisha zikiwa zimechafuka sana.

## Kuweka kabati la vitabu nyumbani



KUNA njia rahisi zaidi ya kuweka kabati la vitabu kwenye ukuta kama moja ya pambo linaloongeza mandhari ya nyumba.

Kabati la vitabu lina faida nyingi likiwa ndani ya nyumba kwani husaidia kuongeza uelewa na taaluma kwa watu wanaoishi ndani.


Hizi ni baadhi ya njia ambazo unaweza kuzitumia kuweka kabati ndani ya nyumba.

**1:** Unaweza kuweka kabati la vitabu kwenye ukuta nyuma ya viti au sofa kwenye sebule.

**2:** Unaweza kujenga kabati kati ya madirisha mawili ya chumbani au sebuleni. Mtindo huu unafanya chumba chako kuwa na mwonekano wa kuvutia hasa nyakati za mchana mwanga unakuwa mkali.

**3:** Pia unaweza kuweka kabati chini ya ngazi inayoelekea vyumba vya juu, hapa utakuwa umetumia vyema nafasi hiyo ambayo mara nyingi haitumiki ipasavyo.

# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO... ...AIBU YA KUOMBA, KUNYIMWA...

# Jaji mkuu ataka Rais Kenyata ang'olewe haraka madarakani

**NAIROBI,** KENYA

JAJI mkuu wa Kenya, Martha Koome, anataka mahakama ya rufaa kutangaza kwamba Rais Uhuru Kenyata amekiuka katiba ya nchi hiyo kwa kushindwa kuwateuwa majaji sita.

Kauli hiyo ameitoa baada ya Rais Kenyatta kukataa kuwateua majaji hao katika orodha ya majaji 40 walioteuliwa na tume ya huduma za mahakama (JSC) miaka mitatu iliyopita .

Koome pia alitaka mahakama itangaze kwamba suluhu ya madai ya kukiuka ni kuondolewa ofisini kwa kiongozi huyo.

Katika rufaa dhidi ya uamuazi wa Mahakama ya juu zaidi, Uhuru Kenyatta aliagizwa kuwateuwa majaji sita na iwapo atashindwa kufanya hivyo Jaji mkuu achukue jukumu la kutekeleza hilo.

Hata hivyo, Koome amekataa kufanya kazi hiyo ambayo ilipaswa kutekelezwa na rais .

Badala yake, amependekeza kutangazwa kiongozi huyo wa juu wa Kenya amekiuka kipengele cha 3(1) na cha 166(1) (b) cha katiba au maagizo.

**BBC**

# Marekani yaishutumu China kwa kuvuruga utulivu

**WASHINGTON,** MAREKANI

WAZIRI wa Ulinzi wa Marekani Lloyd Austin, ameishutumu vikali China kwa kile alichokiita kufanya shughuli za kijeshi za kichokozi katika maeneo ya karibu na Taiwan.

Pia ameonya taifa hilo kuongeza vitendo vya kichokozi katika ukanda mzima wa Asia-Pasifiki.

Akihutubia mkutano wa kilele wa usalama wa Shangri-La Dialogue huko Singapore, ambao unahudhuriwa na mawaziri wa ulinzi wa eneo la Asia na sehemu nyingine duniani, Austin alisema vitendo vya kutishia usalama vimeongezeka.

Alisema China imefanya kile kinachoonekana kama uvamizi mara kadhaa katika eneo la ulinzi wa anga la Taiwan mwaka huu.

Waziri wa Ulinzi wa Taiwan, Wei Fenghe alimtahadharisha Waziri Austin kwamba China iko tayari kuingia vitani ikiwa kisiwa hicho kitajitangazia uhuru wake.

Mivutano kati ya serikali ya Marekani na China inazidi kuongezeka kuhusu kisiwa cha Taiwan ambacho kinajitawala chenyewe kidemokrasia, lakini kwa upande wa China inakichukulia kama eneo lake na kudhamiria kukiteka siku moja, ikilizimka hata kwa mabavu

**DW**

# Mapigano Severodonetsk sasa mtaa kwa mtaa

**KYIV,** UKRAINE

MAPIGANO makali yamesambaa mitaani katika mji muhimu wa Ukraine Severodonetsk, kati ya wanajeshi wa pande mbili Ukraine na Russia.

Ripoti mpya iliyotolewa na Wizara ya Ulinzi ya Uingereza, ilisema kuna idadi kubwa ya wanajeshi waliojeruhiwa na kuawa katika mapigano hayo yanayoendelea.

Hata hivyo, taarifa hiyo ilieleza vikosi vya Russia vimeweza kupata mafanikio ya kusonga mbele katika mji wa kusini.

Iliongeza kuwa vikosi vya Russia vinafyatua makombora mengi ya ardhini na ya anga, katika jaribio la kuyazidi uwezo majeshi ya Ukraine.

Wizara hiyo ilisema inapungukiwa na makombora ya kisasa na imeamua kutumia mfumo wa kuzuwia makombora mazito dhidi ya maeneo yanayolengwa nchini Ukraine ambayo kwa kawaida yametengenezwa kwa ajili ya kuangamiza mifumo inayobeba ndege kwa kutumia mitambo ya ufyatuzi wa nyuklia.

RAIS UMOJA WA ULAYA AWASILI KIEV

Rais wa Halmashauri Kuu ya Umoja wa Ulaya, Ursula von der Leyen, jana aliwasili mji wa Kiev nchini Ukraine kwa ajili ya majadiliano kuhusu ombi la nchi hiyo kujiunga na umoja huo.

Kiongozi huyo amepanga kujadili masuala ambayo hayajaweza kupatiwa ufumbuzi katika ombi la Ukraine lililowasilishwa kwenye umoja huo na Rais Volodymyr Zelensky.

Hadi Ijumaa ijayo Von der Leyen anatarajiwa kutangaza tathmini yake ya kama Ukraine itapata hadhi ya kuwania nafasi hiyo katika Umoja wa Ulaya.

Ziara hiyo ni ya pili kwa kiongozi huyo kwenda Ukraine tangu kuanza kwa vita mwezi Februari.

Aprili alilitembelea eneo la Bucha, kitongoji cha Kiev, eneo ambalo kuligundulika miili ya mamia ya watu baada ya majeshi ya Russia kuondoka katika eneo hilo.

**UKRAINE IMESEMA WATOTO 24 ZAIDI WAMEKUFA MARIUPOL**

Ofisi ya mwendesha mashtaka ya Ukraine, jana ilisema kuwa imebaini vifo vya watoto wengine 24 zaidi katika mji wa bandari wa Mariupol.

Mji huo uliwekwa katika mzingiro na majeshi ya Russia kwa majuma kadhaa kabla ya kuuteka kabisa katikati ya Mei.

Kwa ujumla ofisi hiyo ilisema takribani watoto 287 wamekufa tangu Russia iivamie Ukraine na wengine zaidi ya 492 wamejeruhiwa.

Taarifa ya ofisi hiyo ya mwendesha mashtaka imetaja sababu za vifo kuwa ni mashambulizi ya jeshi la Russia.Hata hivyo shirika la habari la Uingereza Reuters, limeshindwa kuthibitisha uhakika wa taarifa hiyo ingawa mapema mwezi huu Umoja wa Mataifa ulisema zaidi ya watoto 250 wameuwawa tangu kuanza kwa vita hiyo na wengine milioni 5 wapo hatarini.

**DW**



Wakazi wa maeneo ya Goma katika jimbo la Kivu Kaskazini wakikimbia mapigano yanayoendelea kati ya waasi wa M23 na wanajeshi wa serikali jana. **PICHA: DW**

# DRC yaishutumu Rwanda shambulio la mizinga

**GOMA,** DRC

JESHI la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, limedai kuwa Rwanda imeishambulia shule kwa mabomu ya mizinga katika eneo lake na kuwaua watoto wawili.

Katika taarifa yake, jeshi hilo lilisema kwamba vikosi vya Rwanda viliyashambulia kwa mizinga maeneo mawili ya Rutshuru katika jimbo la Kivu Kaskazini siku ya Ijumaa mchana. Taarifa hiyo ilisema kuwa watoto waliouawa walikuwa na umri kati ya miaka 6 na 7 na mwingine amejeruhiwa katika shambulio hilo.

"Mbali na idadi ya watu, jeshi la Rwanda lililipua shule nzima kwa mabomu. Hili linachukuliwa kuwa uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya binadamu," ilisema taarifa hiyo.

Madai hayo yanafuatia kauli iliyotolewa na wizara ya ulinzi ya Rwanda juzi kwamba jeshi la Congo lilirusha maroketi mawili ndani ya eneo lake.

Kwenye taarifa yake, wizara ya ulinzi ya nchi hiyo ilisema kuwa jeshi la DRC, lilirusha roketi mbili hadi Rwanda kutoka eneo la Bunagana, magharibi mwa nchi hiyo majira ya saa sita mchana.

Aidha taarifa hiyo ilisema mashambulizi ya aina hiyo ya makombora ya vikosi vya DRC yalifanyika Machi 19 na Mei 23 na kusababisha hasara na kuharibu mali.

Shutuma hizo zinatolewa wakati uhusiano wa mataifa hayo jirani ukizidi kuzorota kwa kasi, kutokana na kuzuka upya kwa wanamgambo wa M23 katika eneo la mashariki mwa DRC ambalo limekumbwa na machafuko.

**DW**

MAKALA

# KATIBA IMARA NI ZAIDI YA UTASHI WA RAIS



Na Magabilo Masambu - 0689157789

MWENYEZI Mungu amekabidhi mamlaka ya kuiongoza dunia hii mikononi mwa watu, lakini watu hawa ni binadamu wanaofanya mema na mabaya kwa sababu ya upungufu wa kibinadamu. Sheria zinatungwa na watu kwa ajili ya kudhibiti huo upungufu unaoweza kusababisha kutenda makosa.

Sheria zinafanya kazi kuu mbili; moja ni kutaka kukinga makosa yasifanyike kwa sababu mtenda makosa anaelewa wazi kwamba 'nikifanya hili nitakabiliwa na mashitaka', ndiyo maana Katiba siyo jambo la siri ili kila mmoja asome aone nini akifanya atakuwa ametenda makosa.

Kazi ya pili ya sheria ni kuhukumu. Baada ya kuwa umekwisha kutenda makosa, sheria inakuwa wazi. Bahati mbaya watu wengi huwatupia lawama mahakimu kwamba wanawawahukumu mahakamani, lakini kwa kweli mahakimu wanafanya kazi ya kusimamia tu kile tulichokubaliana wenyewe kwa maana ya katiba na sheria za nchi.

Sheria inasema ukitenda hivi, adhabu yake ni hii hivyo, ikithibitika bila shaka mbele ya mahakama unahukumiwa siyo na hakimu, bali sheria.

Kwa muda sasa tumekuwa mjadala kuhusu ama mabadiliko ya katiba ama katiba mpya, naona wengine wanadai tume huru ya uchaguzi, yaani mambo ni mengi muda ni mfupi.

Mimi pia ni miongoni mwa watu wanaoamini kwamba, mabadiliko ya katiba ni muhimu sana kwa ajili ya manufaa yetu sote bila kujali tunatoka chama kipi, dini ama kabila gani, kwani upungufu wa katiba unapotokea unatugusa sote.

Angalu uongozi wa awamu ya tano uliweza kutuonyesha mahala pabovu na tunapaswa kuushukuru sana kwa sababu pengine tusingegundua kwa urahisi udhaifu wa katiba tuliyonayo.

Hivi karibuni tumesikia kwamba, Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Bara, Tundu Lissu amelipwa mafao yake na kwamba sasa taratibu zinafanyika ili aweze kulipwa gharama za matibabu. Kama tunavyofahamu kwamba Lissu alishambuliwa na wanaoitwa wasiojulikana akiwa katika majukumu yake ya kibunge Septemba 7, 2017 jijini Dodoma.

Kwanza nitumie fursa hii kuipongeza kwa dhati kabisa serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, imefanya jambo la utu, uungwana lakini zaidi hofu ya Mungu maana kwa kweli kwa mazingira yaliyomtokea Lissu na dunia ikashuhudia hakustahili kutendwa kama alivyotendewa.

Sisi kama nchi moja, tumeishi kwa upendo tangu uhuru. Upendo na umoja wetu ndiyo ulisaidia kuunga mkono juhudi za ukombozi wa nchi za wenzetu hasa kusini mwa Afrika, hatukustahili kutendeana haya.

Pongezi ya pili ni kwa Rais, kama tunavyofahamu Rais Samia akiwa Makamu wa Rais, alikuwa miongoni mwa viongozi wachache waliomtembelea Lissu akiwa Kenya kwa matibabu. Kwa hiyo utu wake ulionekana toka mwanzo na leo amekuwa Rais, amefanya kilichostahili kufanywa, hongera sana mama!

Pamoja na pongezi hizo kwa serikali, jambo muhimu linalobakia ni je, sheria zilizotumika sasa kumpatia Lissu mafao na stahiki zake nyingine kwa wakati huo hazikuwapo? Jibu bila shaka zilikuwapo, lakini utashi wa viongozi tu ukamtuma kwamba hapana na hivyo akakosa stahiki zake kwa kipindi chote hicho.

Ni dhahiri kwamba, kama asingepatikana Rais mwenye utashi wa kutambua kwamba mtu huyu anastahili huduma hizo kama haki yake ya msingi kwa mujibu wa sheria za nchi yetu, basi hata hizo haki zake zingekuwa ndoto na hii ni kwa sababu katiba haimlazimishi Rais kutii sheria kwa sababu yeye ndiye msemaji wa mwisho kwa mujibu wa Katiba ya nchi.

Ibara ya 46(1) na (2) ya katiba yetu inampatia Rais kinga ya kutoshitakiwa, maana yake hili pekee linampa uwezo wa kufanya lolote bila kujali chochote, isipokuwa utashi wake utakavyomtuma katika kuamua mambo bila kulazimishwa na sheria za nchi.

Tunapozungumza juu ya mamlaka ya Rais, tunamzungumzia yeyote atakaye kuwa Rais, leo tunaye Rais mwema, kesho tunaijua?

Kuna wakati hatuamini kwamba mambo haya yanaweza kutupata sisi kwa kuwa sisi ndiyo wenye mamlaka, lakini mambo yanabadilika.

Tanzania hatukuwahi kuamini kama ipo siku tutampata Rais mwanamke kwa sababu ya mfumo dume tulionao, lakini ya Mungu mengi, leo tunaye mama yetu anatuongoza vyema kabisa na mwenyezi Mungu amwongezee umri zaidi aendelee kuupiga mwingi!

Mbuyu ulikuwa kama mchicha, leo tunaweza kuvidharau vyama fulani kesho vikashika madaraka kama ambavyo imetokea kwa baadhi ya nchi hapa Afrika halafu katiba ikiwa imebaki hivi ilivyo kutakuwa na usalama kweli?

Binadamu tunajua tunakotoka lakini kesho yetu anaijua Mungu. Tunaweza tusione umuhimu leo kwa sababu tuliyenaye leo anatenda tunayopenda kesho wote tunaweza kuishia kulalamika tena.

Matumani na imani yangu ni kwamba kwa jinsi ninavyoona mwelekeo na nia njema ya Rais Samia, tunaweza kupata katiba bora siyo katiba mpya.

Jambo la msingi ni kushirikiana naye kwa nia njema, huku tukitambua kwamba nchi hii ni yetu sote, tunahitaji kuijenga kwa pamoja, tuweke pembeni maslahi yetu binafsi na ya vyama vyetu kwa sababu hatujui kesho tutaongozwa na nani, vinginevyo ipo siku tutalia wote na tutakosa wa kutufuta machozi.

**0689157789**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Siri ya kifo cha utata cha mwanamuziki Gobby wa Makassy



Na Adam Fungamwango

ILIKUWA ni Septemba 27 mwaka 1977 pale mashabiki wa muziki wa Tanzania na Afrika Mashariki na Kati kwa ujumla walipopata mshtuko juu ya kifo cha mwanamuziki aliyeanza kuwa staa wa bendi ya Orchestra Makassy, Isihaka Gobby.

Nchi ilizizima kwa vilio na majonzi baada ya mwanamuziki huyo kijana kutoka Zaire (sasa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, mwenye umri wa miaka 28 tu kutagazwa kufariki akiwa ndiyo kwanza anaanza kuwa maarufu kutokana na sauti yake nzuri na uwezo wake mkubwa wa kucheza na kuchangamsha jukwaa, lakini kwa utanashati wake.

Kilichozidisha majonzi na taharuki wakati huo ambapo hakukuwa na mitandao ya kijamii ni aina ya kifo cha mwanamuziki huyo ambaye aliuawa kwa kuchinjwa kama kuku.

Kwa wale wanaolijua lilipo kaburi la msanii Steven Kanumba ambaye alifariki Aprili 7, 2012 akiwa na umri kama huo wa miaka 28, kaburi ya Gobby lipo jirani kabisa na msanii huyo kwenye Makaburi ya Kinondoni, Dar es Salaam.

Ukifika kwenye kaburi lake hata leo utaona yameandikwa maandishi ya Kifaransa, huku kukiwa na jina lake kamili, kuzaliwa na kufariki kwake.

Juu ya kaburi kuna jina la Isihaka Baharia Gobby, jina la bendi Orchestra Makassy, alizaliwa Agosti 22, 1950 na kufariki Septemba 27, 1977.

Mwanamuziki huyo ndiyo kwanza alikuwa ametoka kurekodi wimbo uliokuwa kwa wakati huo umeanza kuvuma wa 'CCM'. Ni wakati ambao vyama vya Tanu na Afro Shirazi vilikuwa vinaungamnisha vyama na kuunda kimoja, hivyo bendi nyingi ziliingia studio na kurekodi nyimbo hizo.

"Twakikaribisha Chama cha Kimapinduzi, kurekebisha hali ya wanyonge, wafanyakazi viwandani, na wale waliopo mashambani, kuweka uchumi wetu mikononi mwetu, Mwalimu Nyerere na Aboud Jumbe msonge mbele msirudi nyuma..." Ni moja kati ya mashairi ambayo alikuwa akiyaimba kwa ustadi mkubwa kwenye wimbo huo.

Wakati huo bendi ya Makassy ilikuwa ikipiga muziki wake kwenye ukumbi wa Hunters Club, Ubungo, ikiwa na ushindani mkubwa kutoka kwa bendi ya Bana Ngenge iliyokuwa katika ukumbi mwingine jirani wa Savannah, na Orchestra Maquis du Zaire iliyokuwa ikipiga katika ukumbi wa Resort Kimara.

Mmoja wa wanamuziki wa bendi hiyo aliwahi kuniambia anakumbuka siku hiyo Gobby jamaa alipochukuliwa kwenda kuuawa.

Ilikuwa Jumapili moja, bendi ya Makassy ilikuwa imetoka kupiga dansi la mchana wamekwisha toka kupiga dansi la mchana la siku hiyo, na alikuwa anaishi naye nyumba moja, lakini vyumba mbalimbali, anasema alikuja mtu mmoja aliyekuwa anafahamiana na marehemu na akamwomba waondoke wote na hiyo ikawa ndio mara ya mwisho kuonekana hai.

Maiti ilikutwa barabara ya Bagamoyo, maeneo ya Kunduchi, ikiwa imechinjwa. Mwanamuziki huyo anasema hakuweza kumtambua mtu huyo kwa sababu yeye alikuwa anapigia bendi ya Western Jazz, hivyo isingekuwa rahisi kumfahamu mtu anayefahamiana na mwanamuziki wa Makassy, hasa akiwa ni Mkongomani, wakati huo ikiitwa Zaire.

Hadi leo hii ninapoandika makala hii, hakuna hata aliyeshukiwa kuhusiana na mauaji hayo, achilia mbali yoyote kukamatwa.

Ingawa hataki kunyoosha maneno moja kwa moja kuhusu hilo, lakini mwanamuziki Kikumbi Mwanzo Mpango Kiki kutokana na tukio hilo lililowahuzunisha na kuwastusha Wakongo wote na bendi zote zilizopo nchini, ndipo alipotunga wimbo wa 'Nasema Sina Ndugu'.

"Nasema sina ndugu wa kuweza kunisaidia, nikifa leo na kesho, maiti ya kwangu bure, yatatupwa kama mbwa na kuyasau pale pale. Wandugu tuwe na huruma, wandugu tuwe na huruma, mateso ya kwangu ni yako, tafadhali tupendane." Ni maneno yaliyo kwenye wimbo huo wa majonzi.

Kama nilivyosema mwanzo kuwa wakati huo hakukuwa na mitandao ya kijamii kama sasa, lakini tukio hilo lilishtua na kutetemesha nchi, hivyo mitaani, vijiweni na maofisini habari ikawa ni ya mwanamuziki huyo kila mtu akisema lake.

Si Kiki, Mzee Makassy mwenyewe, hata mwanamuziki yoyote wa Kikongo, pamoja na kuhuzunishwa na kukerwa na mauaji yale, lakini wameshindwa kuwa wazi ni nani hasa aliyefanya jambo kama lile, ingawa wanakiri kuwa aliuawa.

Wengi walihusisha kifo hicho na mambo ya mapenzi. Wengine wakasema kuwa jambo hilo liliwahusisha Wakongomani wenyewe kwa wenyewe, yaani mwanamuziki huyo alikuwa na uhusiano wa kimapenzi mmoja wa mpenzi wa mabosi zake ambao walikuwa na nyadhifa kubwa.

Inasemekana kuwa hiyo ndiyo sababu iliyofanya kesi hiyo ikaisha kidiplomasia.

Marehemu Gobby alikuwa mwimbaji, mchezaji mzuri sana na mtanashati.

Alikuwa na staili yake moja ya kucheza na kurusha mguu kuzunguka stendi ya maiki na wakati mwingine kufanya kama anajikata ngwala na kupiga hatua za upesi upesi kama anakimbia huku kasimama pale pale alipo.

Aina hiyo ya uchezaji inafanana sana na wanamuziki wa zamani wa Zaiko Langalanga Evoloko Jocker na Mbuta Mashakadokwa wale ambao wamebahatika kuwaona laivu au kwenye video zao.

Staili na vituko hivyo vya Gobby, kama viliweza kuwastaajabisha mashabiki wanaume kwa namna ile basi aliweza kuteka macho na nyoyo za kina dada kwa namna nyingine zaidi.

Kifo cha mwanamuziki huyo ndiyo kilisababisha Mzee Makassy kurudi Zaire kutafuta mwanamuziki mwingine wa kuziba pengo, akarejea na mpwa wake, Remmy Ongalla 1978.

Bendi ya Orchestra Makassy chini ya Mzee Makassy, iliingia nchini ikitokea Uganda ikitwa Jamboz mwaka 1975 ilianza kupiga katika sehemu mbalimbali Dar es Salaam ikiwemo ukumbi maarufu wa New Africa, Hunters Ubungo ambao ndiyo ulikuwa ndio ukumbi wa nyumbani, wakipita wanamuziki maarufu kwa nyakati tofauti kama Mosesengo Fanfan, Gobby mwenyewe, Dingituka Molay 'Nyama ya Nyani', Mbombo wa Mbomboka, Tshimanga Kalala Assosa, Remmy, Maliki Star, Adam Seye na wengine wengi

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na wanapomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-5

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

NDIPO alipogundua kuwa yote yale ambayo alikuwa akifanyiwa akiwa mdogo. Kuishi kwa kufichwafichwa, kufundishwa ujasiri, kutojichanganya na watu, ukakamavu pamoja na kufundishwa jinsi ya kutumia silaha, ilikuwa ni kuimarishwa ili kulipiza kisasi.

"Ahsante baba kwa kunifunulia yaliyojificha. Umekaa na kidonda hiki kwa muda mrefu. Leo umeamua kunifunulia nikione. Nakuahidi sitokuangusha. Nitawamaliza wote waliomuua mama yangu mzazi. Alikuwa anaitwa nani?"

"Jina lake kamili lipo nyuma ya hiyo picha." Alijibu mzee Pokwa na kumpa mkono kijana wake.

"Umekua sasa mwanangu. Wakati naanza mkakati huu sikutegemea kama utafanikiwa. Nilidhani utakuwa mtoto goigoi. Ndiyo maana nilitumia nguvu sana kukuandaa. Kuna wakati nilijua nitashindwa, lakini sasa najivunia nimepata mtoto jasiri."


"Anayefuata ni nani?" Prince akauliza kwa hasira.

"Tulia kwanza kijana wangu, usiwe na hasira sana. Kazi hii haihitaji hasira. Ukiwa na hasira utaharibu. Hutoweza kufanya kazi kwa ufanisi."

Alipomaliza kuongea maneno hayo, aliinuka, na kwenda kwenye kabati kubwa. Aliporejea alikuwa na picha ya mtu mwingine. Akamkabidhi kijana wake kama kawaida.

"Huyo anaitwa mzee Hassan. Huyu miaka mingi iliyopita wakati mama yako yu hai alikuwa kijana sana. Huyu ana hoteli yake kubwa pale Manzese Argentina. Huwa anafika pale kuanzia saa tatu usiku kukusanya pesa za mauzo ya siku. Inaitwa Upendo Hotel, iko kwenye kona tu ya barabara ya kwenda Tandale na ile kubwa ya Morogoro, wala huwezi kuipotea." Mzee Pokwa alitoa maagizo.

"Onyo. Ni kwamba utakapofanya kazi yako ya kuiondoa roho ya




**"Umekua sasa mwanangu. Wakati naanza mkakati huu sikutegemea kama utafanikiwa. Nilidhani utakuwa mtoto goigoi. Ndiyo maana nilitumia nguvu sana kukuandaa. Kuna wakati nilijua nitashindwa, lakini sasa najivunia nimepata mtoto jasiri."**

mzee huyu usijaribu kuchukua kitu chochote kutoka kwake. Utajua mwenye utamuua kabla ya kuchukua pesa zake za mauzo au baada. Lakini kama ukimaliza kazi yako usijaribu kuchukua pesa. Wewe siyo mwizi wala jambazi. Wewe unalipa kisasi tu. Wanaolipa kisasi huwa hawachukui kitu chochote kile kwa mtu anayehitajika kufa zaidi ya roho yake tu. Vinginevyo unatafuta mkosi ambao utakuandama. Wewe unalipa kisasi ambacho ni haki yako, lakini kuchukua pesa, kitu chochote mkufu, saa simu ya mkononi ambayo hakihusiani na kisasi ni mbaya sana."

"Sawa baba nimesikia."

"Nataka kazi hii uifanye kesho usiku, leo pumzika ujiandae, sawa?"

"Nimekuelewa baba' angu."

***************************

Mchezo alioufanya haukutofautiana na ule alioufanya kule Ilala Bungoni, gari alilipaki Manzese kwa Bakhresa, karibu kabisa na daraja la juu la watembea kwa miguu, ambalo unaweza kusema ni la kwanza hapa nchini kujengwa, kabla ya haya mengine tunayoyaona.

Alipoangalia simu yake ilimfahamisha kuwa ni saa tatu kasorobo. Akakumbuka aliambiwa na baba yake kuwa mzee Hussein hufika saa tatu kwenda kuchukua pesa zake.

Alitembea taratibu akifuatana na baadhi ya watu waliokuwa wakirejea nyumbani kwao baada ya mishughuliko ya mchana kutwa.

Moja kati ya watu aliofuatana nao walionekana ni mke na mume waliokuwa wakigombana. Kwa sababu hakuwahi kuishi kwenye familia aliona ni kitu cha ajabu.

Mke alikuwa amebeba mtoto na baba anatembea huku akiongea maneno ambayo yalionekana kabisa alikuwa anataka amuachishe mtoto kunyonya. Lakini mama alikuwa hataki.

"Yaani mtoto mwaka mmoja na nusu baba Beka tumuachishe kweli?" Alilalamika mke.

"Ndiyo nimeshasema hivyo."

"Aka mwenzangu, mtoto bado huyu, kliniki wamesema mtoto anyonye maziwa ya mama hadi miaka miwili."

"Hakuna, kwani umeolewa na kliniki au mimi?" Mume alizidi kukoroma.

"Kule kuna madaktari na manesi, ni watu wa afya wanajua kila kitu." Mke alitetea.

"Sasa endelea kuwasikiliza, watakuponza."

"Eee eee bwana, usinitishe, kama unataka kwenda kwa huyo Asha wako nenda."

Mwanaume alitaka kuongea kitu, lakini akapatwa na kigugumizi.

Prince alikuwa nyuma yao, hivyo aliwaona wote wawili vizuri. Mwanaume kwa hasira alitaka kumpiga mkewe ambaye alikuwa na mtoto.

Kabla mkono haujatua mwilini, ghafla Prince aliruka kwa hatua ndefu na kuukamata, kabla haujafika kwenye shavu.

"Hallo, wewe ni mwanaume, unagombana vipi na mkeo njiani kama hivi?" Kwa jinsi alivyoushika mkono huo, baba yule hakutamka kitu chochote. Wala hakutaka ugomvi na yeye. Ni kwamba alikutana na mkono wa binadamu mithili ya chuma. Aliona kabisa huyu mwamba ni mtu wa mazoezi.

"Mama, huyu kama akikufanyia fujo tena njiani au nyumbani, au akataka kukulipizia kisasi changu kwa kukusaidia, basi kesho njoo pale kwenye duka lile lenye picha ya Bruce Lee."

"Sawa baba, maana mume wangu siku hizi simuelewi, ananipiga mara kwa mara, kisa nimuachishe mtoto kunyonya, hajafika miaka miwili huyu, mimi akinipiga nitakuja kwako mdogo wangu."

"Siyo kukupiga, hata akiendelea na mpango wake wa kutaka kumuachisha mtoto kunyonya, we njoo, halafu ndiyo atanijua mimi nani."

Wakati Prince akiongea na mama yule mumewe alikuwa kimya. Alishaingiwa na woga kuwa amekutana na mtu mkakamavu na si wa kawaida.

Alijua anaongopa, hafanyi kazi pale alipomwambia, ila aligundua kuwa jamaa alishamhofia, hivyo kwa kitendo cha kumwambia tu mkewe akikukorofisha aje sehemu ile, alijua hatorudia tena kumpiga na kumnyanyasa.

"Haya nendeni. We bwana, nikiona mkeo kaja kesho au siku yoyote pale dukani kwangu kuniambia kuwa umempiga au kumtukana, ndiyo utanijua

ITAENDELEA JUMAPILI



# Watanzania wasubiri kuona tabasamu la Profesa Jay

WATANZNIA wana hamu ya kumuona mwanamuziki wao kipenzi, Profesa Jay, akiwapungia mkono na kutabasamu. Lakini swali lao kuu ni lini ndoto hiyo itakuwa kweli?

Jibu sahihi lipo kwa ndugu wa rapa huyo mwanzilishi wa muziki wa Bongo Fleva, ambao hivi karibuni walijitokeza na kueleza Profesa Jay yupo vizuri baada ya kuruhusiwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ambako alikuwa akitibiwa kwa muda mrefu.

Hata hivyo, walisema kwa sasa si rahisi watu kumuona kutokana na kuhitaji muda kupumzika kutokana na matatizo anayokabiliana nayo.

Mke wa Professor Jay, wakati akifafanua kauli ambayo ilitolewa na familia kwamba rapa huyo mkongwe hajapelekwa nyumbani bali kwenye makazi maalum, alisema mume wake kiakili yupo sawa na kwenda huko si kwa ajili ya kurudishwa sawa.

Amesisitiza kwamba kwenda sehemu nyingine ni kufanya mazoezi ya viungo kutokana na kulala ICU kwa miezi mitatu.

Hata hivyo, hawajui ni muda gani afya yake itakuwa imeimarika kabisa.

# Justin Bieber apooza uso

STAA wa muziki kutoka nchini Canada, Justin Bieber amethibitisha kuwa na tatizo la kupooza usoni kutokana na ugonjwa wa Ramsay Hunt.

Tamko hilo amelitoa siku chache tu baada ya kutangaza kusimamisha ziara yake ya kimuziki.


Mwanamuziki huyo (28) alitumia ukurasa wake wa Instagram kwa kuweka video ya dakika tatu akielezea ugonjwa huo ambao ni matatizo ya shingo ambayo yanaweza kusababisha kupooza uso.

Jicho la kulia la Justin haliwezi kupepesa na upande wa kulia wa uso wake haufanyi kazi alisema.

"Nilitaka kuwajuza kuhusu kile kinachoendelea kama unavyoweza kuona uso wangu. Nina ugonjwa huu uitwao Ramsay Hunt syndrome na ni kutokana na virusi hivi ambavyo hushambulia mishipa ya fahamu katika sikio langu na mishipa yangu ya uso na kusababisha kupooza.' Alisema.

Aliongeza 'Siwezi kuamini, nimefanya kila kitu ili kupata nafuu lakini ugonjwa huu unazidi kuwa mbaya, Moyo wangu unaniuma kwamba nitalazimika kuahirisha ziara yangu kutokana na maagizo ya madaktari".





HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ARSENAL YAMTAKA SAVIC

ARSENAL wako tayari kulipa zaidi ya pauni milioni 42 kwa ajili ya kiungo wa kati wa Lazio, Mserbia Sergej Milinkovic-Savic, 17, ingawa Newcastle wanaweza pia kuweka dau kwa ajili ya mchezaji huyo. ***(Corriere dello Sport)***

### ZIDANE AITWA PSG

PSG wanajaribu kumshawishi kocha wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane, 49, kuchukua nafasi ya Mauricio Pochettino kama kocha wao mpya. ***(ESPN)***

### POGBA ANASUBIRI

PAUL Pogba bado hajakamilisha mkataba wake wa uhamisho huru wa kutoka Manchester United kuelekea Juventus, huku kiungo huyo wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 29, akisubiri kuona iwapo Zinedine Zidane anateuliwa kuwa kocha mpya wa Paris St-Germain. ***(RMC Sport)***

### KOUNDE ANAONDOKA

KLABU ya Sevilla imesema Jules Kounde anaangalia uwezekano wa kuondoka katika klabu hiyo msimu huu, huku Chelsea ikitarajiwa kumpa mkataba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Sport Witness)***

### JESUS AGOMBEWA

AC Milan ndio klabu ya hivi karibuni kabisa kuonesha nia ya kutaka kumsajili Mbrazili wa Manchester City, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 25. ***(90min)***

### MARQUINHOS SAFI ARSENAL

ARSENAL wako tayari kutangaza kumsajili mshambuliaji Mbrazili mwenye umri wa miaka 19, Marquinhos kutoka klabu ya Sao Paulo kwa mkataba wa miaka mitano kwa malipo ya takriban pauni milioni 3. ***(Guardian)***

### RAPHINHA AWA LULU

KLABU ya Arsenal ni miongoni mwa klabu zinazoangalia uwezekano wa kumchukua - mchezaji wa Leeds United, Raphinha msimu huu, huku Barcelona, Manchester United, Chelsea na Liverpool zikihusishwa pia na winga huyo Mbrazili mwenye umri wa miaka 25. ***(Telegraph)***

### LIVERPOOL HAIJAKUBALI

LIVERPOOL bado haijakubali gharama kwa ajili ya mshambuliaji wa Benfica, Darwin Nunez, blakini Muruguay huyo mwenye umri wa miaka 22 tayari amewaambia marafiki zake na familia yake anahamia Anfield. ***(Echo)***

### LUKAKU NA INTER

UHUSIANO wa mmiliki mpya wa Chelsea, Todd Boehly na kampuni ya rapa wa Marekani, Jay-Z, Roc Nation Sports unaweza kuwa ni muhimu Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 29, kurudi tena Inter Milan. ***(Telegraph)***

### JOAO AWINDWA

JOAO Palhinha, 26, wa Sporting Lisbon amebakia kuwa mchezaji anayelengwa zaidi na Wolves licha ya nia ya Fulham kwa kiungo huyo wa kati raia wa Ureno. ***(MailOnline)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# FRENKIE DE JONG NJIA NYEUPE MAN UNITED

●●● Afikia makubaliano kutua Old Trafford kuungana na kocha Ten Hag, Xavi apambana...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United ina uhakika wa kufikia makubaliano na Barcelona kwa ajili ya kumsajili kiungo, Frenkie de Jong baada ya mazungumzo kati ya klabu hizo mbili kuanza, kwa mujibu wa 90min.

United wametumia muda mwingi wa wiki iliyopita katika mazungumzo na wawakilishi wa De Jong mwenye umri wa miaka 25 na makubaliano mapana kuhusu maslahi binafsi ambayo yameshafikiwa baada ya mchezaji huyo kuthibitisha kuwa ana furaha kuhamia kule Old Trafford.

Kocha mpya, Erik Ten Hag amefanya mazungumza binafsi na De Jong na amemshawishi nyota huyo wa zamani wa Ajax kujiunga nae.

**Baada ya Man United kufikia makubaliano na De Jong, waliingia kwenye mawasiliano ya moja kwa moja na Barcelona na klabu hizo mbili ziko kwenye mazungumzo.**

Kocha wa Barca, Xavi pia amezungumza na De Jong na kumwambia kuwa angefurahi kama angebaki, lakini hali ya kifedha ya klabu hiyo inamaanisha kuwa ni mmoja wa wachezaji ambao wako tayari kuchukua ofa.

Miamba hao wa Katalunya wameweka wazi kwa United kwamba, watahitaji kulipwa karibu euro milioni 75 pamoja na ziada ya karibu euro milioni 10 ili kumuachia nyota huyo wa Uholanzi, ingawa ofa ya sasa ya Mashetani Wekundu ni euro milioni 70 ikijumuisha na nyongeza.

Kwa mujibu wa 90min, vyanzo kutoka kwa klabu zote mbili kuna imani kwamba dili hilo litakuwa tayari kwa De Jong kufanyiwa vipimo vyake vya afya mwishoni mwa mwezi huu.

Wakiwa wamemkosa Darwin Nunez ambaye amefikia makubaliano na Liverpool, United wanahangaika kumpata De Jong ili kuimarisha kikosi chake chini ya kocha Ten Hag, ambaye aliweka wazi hata kabla ya kuteuliwa kuwa mchezaji huyo wa Barca ndiye alikuwa shabaha yake kuu ya uhamisho.

LIVE IN PLAY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 253,

MECHI KALI

SWITZERLAND

VERSUS

PORTUGAL

1 | 3.39

X | 3.44

2 | 2.06

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:

18+ 0764115588, 0677115588 0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BALE HAJAAMUA WAPI ATACHEZA



**CARDIFF,** Wales

MSHAMBULIAJI wa Wales, Gareth Bale hataharakisha kufanya maamuzi kuhusu mustakabali wa klabu gani atacheza msimu ujao, lakini amekataa kabisa kuhamia Getafe inayoshiriki Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.


Bale atakuwa mchezaji huru mwishoni mwa mwezi huu wakati mkataba wake na Real Madrid utakapofikia mwisho, ambapo ametumia miaka tisa iliyopita akicheza pale Santiago Barnabeu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 amekuwa akihusishwa na Klabu kadhaa za Ulaya na Marekani, mojawapo ikiwa ni Getafe yenye maskani yake jijini Madrid.

Akizungumza mapema wiki hii, rais wa Getafe, Angel Torres alidai kuwa timu hiyo ya Hispania iliwasiliana na wawakilishi wa Bale kuhusu uwezekano wa kuhamia hapo.

Hata hivyo, Bale alikanusha wakati alipokuwa akizungumza kwenye mkutano na waandishi wa habari ambao alitawaliwa na maswali kuhusu uhamisho wake ujao.

Alipoulizwa kama anakaribia kufanya uamuzi, mshambulizi huyo wa zamani wa Tottenham Hotspur alicheka na kusema: "Hapana. Sitaenda Getafe, hilo ni la uhakika.



## AC Milan mbio kumwania Jesus

**MILAN,** Italia

KLABU ya AC Milan imeingia kwenye mbio za kuwania saini ya mshambuliaji wa Manchester City, Gabriel Jesus.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2023 na mazungumzo juu ya mkataba mpya pale kwenye uwanja wa Etihad yameshindwa kufikia makubaliano.

Kwa mujibu wa 90min, Man City bado wanataka kumbakiza Jesus kwa mkataba mpya na wanatumaini ofa waliyompa anaweza kuikubali.

Kocha Pep Guardiola anaamini pia amemuonesha Jesus jinsi anavyomheshimu mchezaji huyo kwa kumuanzisha katika kila mechi kuu ambayo klabu ilikuwa nayo kuelekea mwisho wa msimu.

Hata hivyo, Jesus mwenyewe na wawakilishi wake wanaangalia ofa nyingine kutoka katika klabu nyingine.

Arsenal wamekuwa makini katika harakati za kumsaka Mbrazil huyo na wanatarajia kumshawishi kuhamia kwao, lakini hawako peke yao, kwani Chelsea, Real Madrid, Barcelona na Juventus nazo zinamuwania.

,545,950

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/06/22 | 21:00 | Plaza Colonia CD vs CA Boston River | 2.70 | 3.10 | 2.46 |
| 02. 14/06/22 | 21:00 | San Lorenzo vs Arsenal Sarandi | 2.34 | 2.95 | 3.00 |
| 03. 15/06/22 | 01:00 | Patronato Parana vs Aldosivi | 2.31 | 3.10 | 2.91 |
| 04. 15/06/22 | 03:30 | Juventude RS vs Santos | 2.27 | 2.89 | 3.18 |
| 05. 15/06/22 | 20:00 | Barracas Central vs Union Santa Fe | 2.45 | 3.04 | 2.75 |
| 06. 15/06/22 | 22:30 | Atletico Tucuman vs Lanus | 2.43 | 3.14 | 2.70 |
| 07. 15/06/22 | 22:30 | Banfield vs Central Cordoba | 2.21 | 3.04 | 3.14 |
| 08. 16/06/22 | 03:30 | Atletico Pr vs Corinthians | 2.24 | 2.90 | 3.24 |
| 09. 16/06/22 | 03:30 | America Mineiro MG vs Fluminense | 2.35 | 3.10 | 3.00 |
| 10. 16/06/22 | 22:15 | Keflavik IF vs Stjarnan | 2.70 | 3.48 | 2.26 |
| 11. 16/06/22 | 23:15 | Valur vs Breidablik | 2.61 | 3.44 | 2.35 |
| 12. 17/06/22 | 03:30 | CA Platense vs Gimnasia y Esgrima | 2.66 | 3.00 | 2.56 |
| 13. 17/06/22 | 03:30 | Racing Club vs Velez Sarsfield | 2.36 | 3.10 | 3.00 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 12/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 2235 | Changchun Yatai vs Dalian Aerbing | 1.35 | 4.33 | 7.87 |
| 14:30 | 3167 | Shijiazhuang vs Chengdu Qianbao | 2.39 | 3.14 | 2.75 |
| 15:00 | 2229 | Kristianstads FF vs IFK Hassleholm | 2.50 | 3.45 | 2.50 |
| 15:00 | 2735 | Forsbacka IK vs IFK Uppsala | 3.74 | 3.88 | 1.74 |
| 15:00 | 5700 | Skiljebo SK vs Raagsveds IF | 2.05 | 3.73 | 2.90 |
| 16:00 | 1219 | IFK Haninge vs Umeaa FC | 2.40 | 3.43 | 2.55 |
| 16:00 | 1509 | Lyn W vs Stabaek W | 2.03 | 3.88 | 2.85 |
| 16:00 | 2611 | LSK Kvinner W vs Arna-Bjornar W | 1.25 | 5.29 | 8.82 |
| 16:00 | 2615 | Northern Ireland vs Cyprus | 1.62 | 3.74 | 5.45 |
| 16:00 | 3660 | Yxhults IK vs IK Gauthiod | 3.30 | 3.95 | 1.90 |
| 16:00 | 4144 | FC Jarfalla vs Kungsangens IF | 2.43 | 3.85 | 2.45 |
| 16:00 | 4620 | Senja FK vs Lorenskog | 6.26 | 5.29 | 1.33 |
| 16:00 | 4967 | Piteaa IF vs Vasalunds IF | 3.53 | 3.53 | 1.87 |
| 16:00 | 5123 | IFK Luleaa vs Kiruna FF | 1.50 | 4.23 | 5.12 |
| 16:00 | 5228 | South Korea U23 vs Japan U23 | 2.46 | 2.86 | 2.91 |
| 16:00 | 5631 | Mvo Wanderers vs Liverpool (URU) | 2.65 | 3.34 | 2.36 |
| 16:00 | 5635 | Roa W vs Valerenga W | 15.71 | 9.82 | 1.07 |
| 16:30 | 1399 | Trygg/Lade vs Innstrandens IL | 2.05 | 3.93 | 2.80 |
| 17:00 | 1764 | Novorizontino SP vs Guarani SP | 2.16 | 2.83 | 3.52 |
| 17:00 | 4675 | Mjolner vs Harstad | 1.25 | 5.72 | 7.89 |
| 18:00 | 3719 | Junkeren vs Steinkjer | 1.05 | 10.84 | 16.76 |
| 18:30 | 1232 | Peka vs Nurmijarven Jalkapalloseura | 2.07 | 3.77 | 2.84 |
| 18:30 | 3488 | Narpes Kraft vs GBK Kokkola | 1.68 | 4.31 | 3.68 |
| 18:30 | 4125 | FF Jaro vs IF Gnistan | 2.06 | 3.33 | 3.19 |
| 19:00 | 3635 | Georgia vs Bulgaria | 1.74 | 3.58 | 4.65 |
| 19:00 | 4737 | Colon Santa Fe vs Union Santa Fe | 2.17 | 2.99 | 3.29 |
| 19:00 | 4804 | North Macedonia vs Gibraltar | 1.05 | 11.11 | 35.36 |
| 19:00 | 5688 | Norway vs Sweden | 2.09 | 3.29 | 3.49 |
| 20:05 | 2374 | Deportivo Madryn vs Belgrano Cordoba | 3.45 | 2.81 | 2.21 |
| 21:00 | 1079 | Altos PI vs Ferroviario CE | 2.65 | 3.09 | 2.50 |
| 21:00 | 4221 | Deportivo Maipu vs San Telmo | 1.54 | 3.63 | 5.69 |
| 21:00 | 5555 | Danubio FC vs Cerro Largo FC | 2.07 | 3.04 | 3.48 |
| 21:30 | 1286 | Godoy Cruz vs Racing Club | 2.55 | 3.09 | 2.60 |
| 21:30 | 1593 | Deportivo Moron vs Villa Dalmine | 2.03 | 2.91 | 3.79 |
| 21:30 | 1898 | Sacachispas FC vs Santamarina | 2.03 | 2.95 | 3.74 |
| 21:45 | 1260 | Greece vs Kosovo | 1.75 | 3.53 | 4.63 |
| 21:45 | 1946 | Spain vs Czech Republic | 1.33 | 4.96 | 8.71 |
| 21:45 | 2123 | Switzerland vs Portugal | 3.39 | 3.44 | 2.06 |
| 21:45 | 3094 | Slovenia vs Serbia | 3.89 | 3.33 | 1.95 |
| 21:45 | 3593 | Malta vs San Marino | 1.15 | 6.67 | 19.20 |
| 22:00 | 1319 | Goias vs Ceara CE | 2.79 | 2.99 | 2.45 |
| 22:00 | 1459 | Sao Paulo vs America Mineiro MG | 1.65 | 3.45 | 4.93 |
| 22:00 | 1892 | Sporting Kansas City vs New England | 2.85 | 3.36 | 2.43 |
| 22:00 | 1897 | Vasco da Gama vs Cruzeiro | 2.61 | 2.81 | 2.76 |
| 22:00 | 2175 | Mitre SdE vs Estudiantes BA | 2.95 | 2.85 | 2.44 |
| 22:00 | 2297 | Atletico Alvarado vs CA Guemes | 2.60 | 2.85 | 2.75 |
| 22:10 | 4370 | Temperley vs Almirante Brown | 2.43 | 2.81 | 3.01 |
| 22:15 | 4860 | Palermo vs Padova | 2.25 | 3.01 | 3.10 |
| 23:00 | 1075 | Envigado FC vs La Equidad | 3.04 | 2.84 | 2.38 |
| 23:00 | 4279 | ABC RN vs Mirassol SP | 2.36 | 3.08 | 2.84 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# KATIBU MKUU AWAPOZA MACHUNGU ZANZIBAR QUEENS

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Fatma Hamad amewataka wachezaji wa timu ya Taifa ya Wanawake Zanzibar (Zanzibar Queens) kutokata tamaa kutokana na matokeo waliyoyapata katika michuano ya Kombe la Cecafa nchini Uganda.

Hamad aliyasema hayo wakati akiwapokea wachezaji hao bandarini juzi wakitokea nchini Uganda kwenye michuano ya Cecafa ambapo Zanzibar ilifanya vibaya katika mashindano hayo.

Alisema kulingana na historia ya nyuma ya timu hiyo ilikuwa ikifungwa mabao mengi zaidi ikilinganishwa na miaka miwili hii ya mashindano haya, hivyo kwa matokeo waliyoyapata wanatakiwa kutovunjika moyo.

**Alisema serikali kupitia Wizara ya Michezo itabuni njia mbalimbali ili kuziwezesha timu za wanawake kuimarika na kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali ambayo Zanzibar inashiriki.**

Alisema ipo mikakati ambayo Wizara itakaa na shirikisho la Soka Zanzibar, ZFF, kuona kwa kiasi gani timu za Wanawake zinapiga hatua kuanzia kwenye ligi za ndani.

"Mmefanya vizuri, mmepambana katika kuipeperusha bendera yenu msivunjike moyo kwa kufanya vibaya kwa kuwa nyote lengo lenu lilikuwa moja la kuhakikisha tunashinda, lakini haikuwa bahati," alisema.

Pia aliliagiza Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar, Kamishna wa Idara ya Michezo Zanzibar kukaa pamoja na ZFF kuona wanatafuta njia ya kuindeleza timu hiyo ikiwemo kupata mechi nyingi ili ipate uzoefu.

Zanzibar Queens katika Michuano hiyo ilifungwa michezo yote mitatu katika kundi B iliyopangwa ambalo lilizikutanisha nchi za Ethiopia, Sudan na Tanzania Bara.




Mkurugenzi wa Masoko wa Benki ya Taifa ya Biashara Tanzania (NBC), David Raymond (wa tatu kutoka kushoto) akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Singida Dk. Binilith Mahenge, mfano wa hundi yenye thamani ya Sh.50 Milioni iliyotolewa na benki hiyo kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa Uwanja wa Soka utakaojengwa eneo la Mtipa nje kidogo ya Manispaa ya Singida. **PICHA: MTANDAO**

# Baseball kwa shule za msingi kuanza

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya watoto wa shule za msingi kwa mchezo wa Baseball yanatarajiwa kuanza kutimua vumbi Juni 18 mwaka huu, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha mkuu wa timu ya Baseball, Kelvin George alisema mashindano hayo yatashirikisha wachezaji kutoka shule 12 zote za mkoa wa Dar es Salaam.

"Lengo la mashindano hayo ni kuhakikisha mchezo wa Baseball unazidi kukua na kufikia hadhi ya Kimataifa kama ilivyo michezo mingine," alisema George.

Alisema kabla ya mashindano hayo kutakuwa na semina ya waamuzi ya siku moja kwa ajili ya kufundishwa mbinu za ufundishaji itakayofanyika Juni 17 mwaka huu.


Alisema kwa sasa mashindano hayo yameanzia mkoani humo na baada ya kumalizika watakwenda kuyafanya kwenye shule za mikoani, lengo ni kuinua vipaji vya vijana.

Aliwataka wazazi kuruhusu watoto wao wajiunge na mchezo huo kwani una faida kubwa ikiwemo kupata fursa ya kwenda kucheza nje ya nchi.

# Michezo

Jumapili Juni 12, 2022

Nipashe

De Jong njia nyeupe Man United UKURASA 21



Mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe (kulia) akifunga bao la kusawazisha dhidi ya Austria kwenye mchezo wa michuano ya ligi ya mataifa ya Uefa baina ya timu hizo, juzi. Timu hizo zilitoka sare ya kufungana 1-1. **PICHA: MTANDAO**

## Vita kali uchaguzi Yanga

**Na Saada Akida**

VITA ya nafasi ya Urais wa Yanga imepamba moto na sasa kuna mchuano mkali kati ya Mwenyekiti wa sasa wa klabu hiyo, Dk Mshindo Msolla na Makamu Mwenyekiti wa usajili, Hersi Said.

Tayari vigogo watatu wamerejesha fomu za kuwania nafasi hiyo na mchakato wa uchaguzi ukitarajiwa kufanyika Julai 10, mwaka huu Dar es Salaam chini ya Mwenyekiti, Ally Mchungahela.

Katika vigogo hao waliochukuwa na kurejesha fomu akiwemo Mwenyekiti wa klabu hiyo Msolla anayemaliza muda wake, naye amejitosa kwenye kinyang'anyiro hicho.

Msolla ambaye amedhamiria kurejea katika nafasi hiyo ili kuendeleza mafanikio yake ndani ya klabu hiyo kwa msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wengine ni Hersi tayari amerejesha fomu kwa kuhakikisha kutaka kuendeleza kile anachokifanya kwa sasa ndani ya klabu hiyo akiwa kama sehemu ya udhamini.

Hersi kwa sasa anafanya kazi kubwa ndani ya klabu ya Yanga ikiwemo suala la usajili na kulipa mishahara makocha na wachezaji ikiwa ni sehemu ya udhamini, lakini ameamua kujitosa kuwania urais.

Mwingine ni Said Barack Kambi ambaye amerejesha fomu kuwania nafasi hiyo huku nafasi ya Makamu wa Rais wamejitokeza wawili ambao ni Arafat Hajji na Suma Mwaitenda ambao wote ni wajumbe wa kamati mbalimbali ndani ya klabu hiyo kwa sasa.

Baadhi ya wagombea nafasi za wajumbe waliorejesha fomu ni Yanga Evarist Makaga, Munir Said Seleman, Alexander Francis Ngai, Mustapha Salum Himba, Omary Kimosa, Seif Gulamali, Ayuob Nyenzi na Saady Khimji.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo wa uchaguzi, Mchungahela alisema zoezi la kurudisha fomu limefungwa juzi (Juni 10) na uchaguzi utafanyika rasmi Julai 10 mwaka huu.

# YANGA, SIMBA SC SASA ZAGONGANA KWA AZIZ KI

**Na Adam Fungamwango**

### ●●● Kila moja yajinasibu kuipata saini ya mchezaji huyo wa ASEC Mimosas, lakini mwandishi wa habari...

KIUNGO mshambuliaji wa Asec Mimosas, Stephen Aziz Ki kwa sasa ndiyo gumzo la mjini, baada ya klabu kongwe nchini Simba na Yanga kudaiwa kupigana vikumbo kuiwania saini yake.

**Tangu juzi, kumekuwa na taarifa kwenye mitandao ya kijamii pamoja na vyanzo mbalimbali vya habari kuwa baadhi ya viongozi wa klabu hizo wamekuwa wakipishana, kupigana vikumbo kuwasiliana naye pamoja na wakala wake ili kumsajili.**

Hata hivyo, hadi sasa hakuna kiongozi yoyote wa klabu hizo, au Maofisa Habari ambao wanataka kuliongelea suala hilo, labda mpaka pale usajili wake utakapokamilika kwenye moja kati ya timu hizo mbili.

Mwandishi wa habari za michezo raia wa Ghana, Micky Junior juzi aliandika kuwa kuna asilimia kubwa mchezaji huyo raia wa Burkina Faso akajiunga na Yanga, jana alikuja na habari tofauti kuwa baada ya kuokena kama anakwenda Yanga, lakini sasa huenda ni Simba.

Kwa mujibu wa chanzo chetu ni kwamba Yanga ambayo imeonekana kufanya jitihada zaidi za kumhitaji kuliko Simba, ilimtengea kiasi cha dola 5,000 za Kimarekani (sawa na Shilingi 11,650,00) za Kitanzania kwenye mashahara wake wa mwezi.

Habari za ndani zinasema kuwa wakala wa mchezaji huyo alitua nchini hivi karibuni na kuongea na viongozi wa Yanga kwenye hoteli moja kubwa na mambo yote yakaenda kama yalivyopangwa.

Pia Makamu mwenyekiti wa usajili wa Yanga, Injinia Said Hersi anatajwa kuwa nchini Ivory Coast kukamilisha mipango ya kumsajili mchezaji huyo.

Hata hivyo, kuna taarifa nyingine kuwa klabu ya Simba imeingilia kati dili la Aziz Ki kwa kuweka kitita cha dola 280,000 za Kimarekani kwa mkataba wa miaka miwili ambazo ni sawa na kiasi cha Sh. Milioni 600 za Kitanzania.

Pamoja na hayo yote, hakuna mwenye uhakika wa asilimia 100 kuwa mchezaji huyo atatua wapi mpaka sasa, kwani viongozi wa timu hizo wameonekana kufanyiana umafia.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa klabu ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again' aliweka video fupi ya mnyama Simba akinywa maji na kuandika maneno yafuatayo.

"Hakuna raha kama kunywa maji na hasa ukiwa na kiu kali au joto kali, moyo huburudika haswa. Muda wa kunywa maji umefika sasa, amkeni amkeni, kumekucha jua limechomoza toka Magharibi, muda utaongea."

Mashabiki wengi wa michezo, wamenasibisha maandishi haya na mambo ya usajili. Mchezaji huyo awali alionekana kwenye mechi ya kwanza Februari 13 mwaka huu, timu yake ikicheza dhidi ya Simba kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Simba ikishinda mabao 3-1, akifunga bao la kufutia machozi, wengi walianza kuvutiwa na uwezo wake.

Hata kwenye mechi ya marudiano Machi 20 mwaka huu, Simba ikichapwa mabao 3-0 dhidi ya ASEC Mimosas, mchezaji huyo alifunga pia bao moja.

Awali Simba ilionekana kumhitaji, lakini baadaye ilionekana kama haina tena haja naye, ambapo Yanga iliingia nayo kuisaka saini yake kabla ya watani zao hao wa jadi kuonekana kurejea tena na kuzua mvutano huo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >